JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO



# MWONGOZO WA KUANZISHA NA KUENDESHA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA

# YALIYOMO

VIFUPISHO ........ iii

UTANGULIZI ........ iv

MALENGO YA MWONGOZO WA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA ........ v

SURA YA KWANZA: DHANA YA SHAMBA DARASA ........ 1

SURA YA PILI: UWEZESHAJI KATIKA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA ........ 5

SURA YA TATU: KILIMO ENDELEVU ........ 21

SURA YA NNE: MASOKO ........ 23

SURA YA TANO: LISHE BORA ........ 29

SURA YA SITA: MASUALA YA JINSIA ........ 31

SURA YA SABA: ZIARA YA MAFUNZO KWA WANAKIKUNDI ........ 33

SURA YA NANE: UFUATILIAJI NA TATHMINI ........ 35

wA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA ........ 35

SURA YA TISA: KUHITIMU MAFUNZO YA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA ........ 42

SURA YA KUMI: UENDELEVU WA MASHAMBA DARASA YA KILIMO BIASHARA ........ 44

VIAMBATANISHO ........ 46

KIAMBATISHO NAMBA 1: KALENDA YA MSIMU ........ 47

KIAMBATISHO NAMBA 2: MFANO WA JEDWALI LA UKADIRIAJI WA GHARAMA ZA UZALISHAJI ........ 50

KIAMBATISHO NAMBA 3A: MFANO WA FOMU YA UCHUNGUZI ........ 51

KIAMBATISHO NAMBA 3B: MFANO WA FOMU YA TAARIFA YA UCHUNGUZI ........ 52

ZANA ........ 53

ZANA NA. 1: ZOEZI LA KUJADILI NA KUFANYA MAAMUZI YA MGAWANYO WAKAZI KATIKA KIKUNDI CHA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA (SDKB) NA FAMILIA ........ 54

ZANA NA. 2: MBINU SHIRIKISHI YA UDHIBITI WA MAPATO NA MATUMIZI YA FAMÍLIA ........ 56

ZANA NA. 3: MBINU SHIRIKISHI YA UDHIBITI WA MAPATO NA MATUMIZI YA FAMÍLIA ........ 57

ZANA NA. 4: PICHA YA MTI INAYOONYESHA AFYA YA BAJETI YA FAMILIA ........ 59

ZANA NA. 5: ZOEZI LA NAMNA SHIRIKISHI YA KUFANYA MAAMUZI KATIKA FAMÍLIA NA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA (SDKB) ........ 62

ZANA NA. 6: FOMU YA UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MWANAKIKUNDI WA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA ........ 65



Sekta ya Kilimo ni kati ya mihimili muhimu ya uchumi wa Tanzania katika kuleta maendeleo ikiwemo kuimarisha usalama wa chakula na lishe. Kilimo husaidia kuongeza kipato kwa wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani na hivyo kuondoa umasikini. Mwaka 2023 Sekta ilikua kwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.3 mwaka 2022. Vilevile, Sekta imechangia asilimia 26.5 katika pato la Taifa kwa mwaka 2023, ikilinganishwa na asilimia 26.2 mwaka 2022.

Kilimo kimetoa ajira kwa wananchi kwa wastani wa asilimia 65.6 na kuchangia asilimia 65 ya malighafi za viwanda. Upande wa mazao ilikua kwa asilimia 4.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 2.7 mwaka 2022, imechangia asilimia 16.2 kwenye pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 15 mwaka 2022 na imeendelea kuchangia asilimia 100 ya upatikanaji wa chakula nchini. Vilevile, mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi katika mwaka 2022/2023 yamefikia takriban dola za Marekani bilioni 2.3 ikilinganishwa na takriban dola za Marekani bilioni 1.2 mwaka 2019/2020.

Pamoja na mchango huo, sekta hii bado inakabiliwa na changamoto kadhaa zinazochangia kuwepo kwa tija ndogo katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo ikiwemo matumizi yasiyoridhisha ya mbinu jumuishi zinazozingatia masuala mtambuka na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini. Ili kuifanya sekta ya kilimo kuwa endelevu, kuongeza tija na usalama wa chakula, Serikali inaendelea kutekeleza miradi na programu mbalimbali ikiwemo Mpango wa Mageuzi ya Kilimo. Mpango huu unalenga kubadilisha sekta ya kilimo kuwa ya kibiashara na shindani, kuongeza ushiriki wa Sekta binafsi, kuboresha miundombinu na huduma za ugani.

Ili kuongeza tija katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo, Wizara imeandaa mwongozo huu kwa ajili ya kuanzisha na kuendesha mashamba darasa ya kilimo biashara ambayo yatawawezesha washiriki kujifunza kwa vitendo, kuendesha shughuli zao kitaalam na kibiashara. Hivyo, mwongozo huu ni nyenzo ya Maafisa Ugani wa Sekta ya Umma na Binafsi, wakulima wawezeshaji na wadau wote wanaoshiriki kutoa mafunzo ya shamba darasa la kilimo biashara nchini. Nitoe rai kwa wadau wote kutumia mwongozo huu katika kuratibu uanzishwaji na uendeshaji wa mashamba darasa ya kilimo.

**Hussein M Bashe (Mb)**
**WAZIRI WA KILIMO**



Mwongozo wa Shamba Darasa la Kilimo Biashara umeandaliwa ili kuwa msingi wa kufundisha wakulima masuala ya kilimo biashara na kwa kufuata mnyororo wa thamani. Lengo la kuandaa mwongozo huu ni kuwaleta pamoja wadau wa Sekta ya Kilimo ili wautumie katika utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima na wadau wengine wa Sekta ya Kilimo.

Ninapenda kuwashukuru wote waliohusika katika uandaaji wa Mwongozo huu wakiwemo Wataalam kutoka **Wizara ya Kilimo, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa – (OR-TAMISEMI), Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE), Chama cha Wagani Tanzania (Tanzania Society of Agricultural Education and Extension - TSAEE) na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA).**

Shamba Darasa la Kilimo Biashara ni mbinu shirikishi inayounganisha shughuli za kilimo katika mnyororo wa thamani. Wakulima hujifunza kuhusu usimamizi wa mazao shambani, ujuzi katika masoko ili kuzalisha kwa kuzingatia na mahitaji ya soko, usawa wa kijinsia, usalama wa chakula na lishe pamoja na ufuatiliaji na tathmini. Mbinu hii inalenga kuimarisha fursa za kiuchumi kwa wakulima na kuboresha maisha yao.

Mbinu hii ya ugani inazingatia mbinu endelevu za kilimo kinachoendana na mabadiliko ya tabianchi. Wakulima hujifunza kuhusu usimamizi endelevu wa rasilimali, kilimo kinachozingatia hali ya hewa na mbinu za uhifadhi wa mazingira. Kwa ujumla, Shamba Darasa la Kilimo Biashara linawawezesha wakulima kupata maarifa na ujuzi wa kufanya maamuzi sahihi ya kilimo endelevu.

Wizara inapenda kutoa shukrani za pekee kwa Washirika wa Maendeleo ikiwemo Shirika la **CARE International** na **Sustainable Agriculture Tanzania (SAT)** kwa kushiriki na kuwezesha maandalizi ya Mwongozo huu.

Ni matumaini yangu kuwa wadau wote watazingatia taratibu, kanuni na maelekezo yaliyomo kwenye Mwongozo huu ili kuleta matokeo chanya katika Sekta ya Kilimo. Mwongozo huu utaanza kutumika mwaka 2024.

**Gerald G. Mweli, ndc**
**KATIBU MKUU**

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **AMCOS** | Agricultural Marketing Co-operative Society |
| **CAN** | Calcium Nitrate. |
| **CARE** | Cooperative for Assistance and Relief Everywhere. |
| **DAP** | Diammonium Phosphate. |
| **FAO** | Food and Agriculture Organization. |
| **GBV** | Gender-Based Violence |
| **ISO** | International Standard Organization |
| **KIKIMATA** | Kilimo Kinachoendana na Mabadiliko ya Tabianchi |
| **NPK** | Nitrogen, Phosphorus and Potassium. |
| **NPS** | Nitrogen Phosphorus Sulphur. |
| **OR – TAMISEMI** | Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. |
| **PPT** | Participatory Performance Track |
| **RA** | Rainforest Alliance |
| **SA** | Sulphate of Ammonia |
| **SACCOS** | Savings and Credit Co-operative Societies |
| **SAT** | Sustainable Agriculture Tanzania |
| **SDKB** | Shamba Darasa la Kilimo Biashara. |
| **SILC** | Savings and Internal Lending Communities. |
| **SUA** | Sokoine University of Agriculture. |
| **TANTRADE** | Tanzania Trade Development Authority. |
| **TBS** | Tanzania Bureau of Standards |
| **TFRA** | Tanzania Fertilizer Regulatory Authority |
| **TOAM** | Tanzania Organic Agriculture Movement |
| **TOSCI** | Tanzania Official Seed Certification Institute. |
| **TPHPA** | Tanzania Plant Health and Pesticides Authority |
| **TSAEE** | Tanzania Society of Agricultural Education and Extension. |
| **TSP** | Triple Super Phosphate. |
| **UVIKO 19** | Ugonjwa wa Virusi vya Korona 2019. |
| **VICOBA** | Village Community Banking. |
| **VSLA** | Village Savings and Loans Association |

# UTANGULIZI

Sekta ya kilimo ni kati ya mihimili muhimu ya uchumi wa Tanzania kutokana na mchango wake mkubwa katika kutoa ajira, kukuza kipato na usalama wa chakula nchini. Mwaka 2023 Sekta ilichangia asilimia 26.5 katika Pato la Taifa, asilimia 30 mapato ya fedha za kigeni, asilimia 65.6 ya ajira kwa Watanzania, asilimia 100 ya usalama wa chakula na asilimia 65 ya malighafi za viwanda.

Ili kuendeleza kilimo, mbinu mbalimbali zimekuwa zikitumika kusambaza na kukuza maarifa, ujuzi na teknolojia kwa wakulima. Mbinu hizi ni pamoja na kutembelea wakulima na kutoa ushauri wa kilimo, kutoa mafunzo ya pamoja hatua kwa hatua shambani (shamba darasa) na mbinu ya wakulima kushauriana wenyewe kwa wenyewe. Shamba darasa ni mbinu kuu ambayo imekuwa ikitumika hapa Tanzania kusambaza na kukuza maarifa na ujuzi kwa wakulima.

Mwongozo wa shamba darasa wa mwaka 2009 toleo la kwanza umekuwa ukitekelezwa kwa kuzingitia kanuni bora za uzalishaji bila kuweka msisitizo kwenye mbinu za kilimo biashara, usalama wa chakula na lishe na masuala mtambuka (jinsia, magonjwa, mabadiliko ya tabianchi) katika mnyororo mzima wa thamani wa mazao ya kilimo.

Uzalishaji usio wa kibiashara katika mnyororo wa thamani ni moja ya chanzo cha Sekta ya Kilimo kukabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo uzalishaji wenye tija ndogo, ukosefu wa soko la uhakika lishe duni kwa jamii, matumizi yasiyoridhisha ya mbinu shirikishi zinazozingatia mbinu na teknolojia himilivu, masuala ya jinsia na kukosekana kwa Mfumo Endelevu wa Ufuatiliaji na Tathmini. Hali hii imechangia kuwepo kwa tija ndogo katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo.

Ili kuongeza tija katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo, Wizara ya Kilimo imeandaa Mwongozo huu kwa ajili ya kuelimisha na kusaidia wawezeshaji kuanzisha na kuendesha mashamba darasa ya kilimo biashara hatua kwa hatua ikijumuisha kuboresha utekelezaji wa Mwongozo wa awali wa mashamba darasa.

# MALENGO YA MWONGOZO WA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA

## Lengo Kuu

Lengo la Mwongozo huu ni kuainisha utaratibu na hatua za kuzingatiwa wakati wa kuanzisha na kutoa mafunzo kwa wakulima kupitia mbinu shirikishi ya Shamba Darasa la Kilimo Biashara kwa Maafisa Ugani Kilimo, Wawezeshaji, Wakulima na Wadau wote katika Sekta ya Kilimo.

## Malengo Mahususi

i. Kuelekeza wadau wa Kilimo utaratibu wa kuanzisha mashamba darasa ya Kilimo biashara; na

ii. Kuelekeza jinsi ya kutumia mbinu shirikishi za kufikisha na kukuza maarifa na ujuzi kwa maafisa ugani, wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa mazao.

## Walengwa wa Mwongozo

Walengwa wa Mwongozo huu ni maafisa ugani/wawezeshaji kutoka taasisi za Umma na Binafsi zinazojihusisha na mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo.

## Mambo ya kuzingatia kabla ya kutumia Mwongozo

Ni muhimu kila mtumiaji wa Mwongozo huu akaelewa vipengele vyote vilivyoainishwa kwenye Mwongozo kabla hajaanza kuutumia. Hii itamsaidia kuwa na maarifa na ujuzi wa namna ya kuanzisha na kuendeleza shamba darasa lenye mlengo wa kibiashara. Hivyo, ni vema watumiaji wa Mwongozo wakapatiwa mafunzo stahiki ili waweze kuelewa na kuzingatia kikamilifu hatua zote katika Mwongozo huu. Ili Mwongozo huu uweze kuwa na tija, ni muhimu watumiaji wakatoa mafunzo hatua kwa hatua kulingana na vipengele mbalimbali vilivyoainishwa kwenye Mwongozo kulingana na mahitaji ya hatua ya mnyororo wa thamani wa zao husika.

# SURA YA KWANZA: DHANA YA SHAMBA DARASA

## 1.1 Historia ya Shamba Darasa

Dhana ya shamba darasa ilianzishwa nchini Indonesia Barani Asia mwaka 1989 na Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (Food and Agriculture Organization - FAO) kwa ajili ya kukabiliana na janga la ukosefu wa chakula lililosababishwa na upotevu wa mazao uliokuwa umetokana na wadudu. Dhana hii ilianza kama mbinu shirikishi ya kudhibiti wadudu hao waharibifu. Mwaka 1990 FAO ilisambaza dhana ya shamba darasa katika nchi za Afrika ikiwemo Tanzania.

Dhana ya shamba darasa Tanzania ilianzishwa kama mbinu shirikishi ya ugani kwa lengo la kuwakutanisha wakulima ili kujifunza kwa vitendo na kusambaza teknolojia. Mbinu hii ilikusudia kumpa mshiriki wa shamba darasa maarifa katika uzalishaji wa mazao yake kwa kuzingatia kanuni bora za kilimo. Katika mbinu hii, shamba lililochaguliwa na wakulima ndiyo darasa ambalo mafunzo yote yanafanyika na kuwafanya wakulima kuwa huru katika kujifunza. Baada ya mafunzo kila mwanakikundi anatakiwa atekeleze kwenye shamba lake la kazi mambo aliyojifunza kwenye shamba darasa. Pia wanakikundi wanaopata elimu hii wanaweza kuwa viongozi kwa wenzao katika kuanzisha na kuendeleza mashamba darasa ili kuifanya mbinu hii kuwa endelevu.

Kutokana na mabadiliko mbalimbali katika tasnia ya kilimo ikiwemo mabadiliko ya tabia ya nchi, mabadiliko ya teknolojia, kiuchumi na kijamii, wadau mbalimbali ikiwemo Khirika lisilo la Kiserikali la CARE International, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) na Wizara ya Kilimo wamendelea kuboresha namna ya uendeshaji wa shamba darasa kwa kujumuisha masuala muhimu katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo kama masoko, usalama wa chakula na lishe, usawa wa kijinsia, mabadiliko ya tabianchi na ufuatiliaji na tathmini katika shamba darasa la kilimo biashara.

## 1.2 Maana ya Shamba Darasa la Kilimo Biashara

Kutokana na historia ya shamba darasa na mapinduzi katika tasnia ya kilimo, katika Mwongozo huu shamba darasa la kilimo biashara ni mbinu shirikishi ya ugani ya kusambaza na kukuza ujuzi na maarifa kwa wakulima na wadau wengine katika hatua ya mnyororo wa thamani ya zao husika iliyoteuliwa kupitia mafunzo ya nadharia na vitendo. Mbinu hii huwapa washiriki fursa ya kujifunza hatua kwa hatua hadi kufikia lengo la mafunzo yaliyokusudiwa.

### 1.3 Umuhimu wa mbinu ya Shamba Darasa la Kilimo Biashara

i. Kujenga mshikamano na mahusiano ya karibu kati ya wawezeshaji na washiriki;
ii. Kuwezesha washiriki kufanya maamuzi wenyewe;
iii. Kupata eneo la pamoja la kujifunzia;
iv. Kujifunza kwa nadharia na vitendo teknolojia mbalimbali katika hatua husika ya mnyororo wa thamani;
v. Kugundua changamoto kupitia uchunguzi shirikishi unaofanyika katika hatua ya mnyororo wa thamani wa zao husika;
vi. Kuwezesha washiriki kutekeleza kwenye maeneo yao ya kazi mambo waliyojifunza;
vii. Kutoa uhuru na ushirikishwaji katika mfumo mzima wa kujifunza;
viii. Kutoa fursa ya kupeana mrejesho baina ya washiriki, wawezeshaji na wadau wengine; na
ix. Inasaidia kufanya uchambuzi na kuendesha shughuli mbalimbali katika mnyororo wa thamani kwa kuzingatia mahitaji ya makundi maalumu na jinsia.

### 1.4 Sifa ya Shamba Darasa la Kilimo Biashara

i. Linapaswa kutoa fursa ya ugunduzi kwa njia shirikishi kwa kujifunza kwenye hatua mojawapo au zote za mnyororo wa thamani;
ii. Liwe na kusudi maalumu la kujifunza;
iii. Liwe na ukubwa wa nusu eka hadi eka moja;
iv. Liwe linawezesha shughuli zote kufanyika katika vikundi;
v. Liwe linatoa mafunzo kwa wanakikundi cha washiriki kati ya 25 – 30 kwa kuzingatia jinsia;
vi. Liwe kwenye eneo linayofikika kwa urahisi na kuwezesha watu wengi kuona na kujifunza;
vii. Linapaswa kutunzwa vizuri;
viii. Lazima kuwe na ukusanyaji wa taarifa mbali mbali. Mfano, taarifa za mavuno, afya ya udongo, udhibiti wa magonjwa na wadudu.

### 1.5 Mambo ya kuzingatia katika kuanzisha Shamba Darasa la Kilimo Biashara.

Mambo muhimu ya kuzingatiwa wakati wa uanzishwaji na uendeshaji wa SDKB yanajumuisha: -

i. Uwepo wa Kikundi cha washiriki wanaojifunza;
ii. Uwepo wa eneo la kujifunzia;
iii. Hatua mahususi ya mnyororo wa thamani uliyochaguliwa na washiriki kwa lengo la kujifunza;
iv. Uwepo wa mwezeshaji mwenye maarifa na ujuzi katika hatua ya mnyororo wa thamani wa zao husika uliochaguliwa;
v. Kuwepo kwa ushirikishwaji katika kufikia maamuzi ya pamoja katika mchakato wa kujifunza; na
vi. Uwepo wa uwajibikaji wa pamoja kwa washiriki katika hatua zote za kujifunza.

# SURA YA PILI: UWEZESHAJI KATIKA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA

### 2.1 Sifa za mwezeshaji katika shamba darasa la kilimo biashara

Mwezeshaji wa SDKB anatakiwa awe sifa zifuatazo:

i. Awe amepata mafunzo maalum ya uwezeshaji wa SDKB na kutambuliwa na Wizra ya Kilimo;
ii. Awe na uwezo wa kuhamasisha wanakikundi kushiriki kwa usawa;
iii. Aewe na uwezo wakufanya mabadiliko pale inabidi katika kuendesha SDKB kulingana na mazingira ya wakati huo mabadiliko ya tabianchi;
iv. Awe na uelewa wa kutosha katika mnyororo wa thamani wa zao husuika;
v. Awe na uwezo wa kuwezesha watu wazima kujifunza kwa kutumia zana sahihi; na
vi. Awe na mbinu za ushawishi na utetezi kwa wadau mbalimbali katika kilimo.

### 2.2 Mambo ya kuzingatia kabla ya kuanza uwezeshaji katika Shamba Darasa la Kilimo Biashara

i. Kuandaa somo husika;
ii. Kuandaa zana za kufundishia kama chati mgeuzo, kadi ya manila na kalamu ya alama;
iii. Kuandaa eneo na mazingira rafiki ya kujifunzia mfano yaliyo na nafasi na hewa ya kutosha; na
iv. Kuwaandaa washiriki kuwa na vifaa vinavyotakiwa kwa ajili ya mafunzo mfano madaftari, kalamu, na vifaa vingine vinavyoendana na shughuli ya wakati huo.

### 2.3 Mambo ya kuzingatia wakati wa uwezeshaji katika Shamba Darasa la Kilimo Biashara

i. Kutumia mbinu shirikishi zinazo thamini mchango wa kila mwanakikundi kwa kuzingatia jinsia, ili kuwafanya wanakikundi kumiliki mchakato wa mafunzo na hivyo kufanya shughuli za shamba darasa kuwa endelevu;
ii. Kuepuka upendeleo kwa kujenga usawa kwa washiriki wote na kutokutoa mifano inayohusiana na mshiriki yeyote kwani hii inaweza kusababisha mshiriki ajisikie vibaya;
iii. Kutambua kuwa washiriki hawana uwezo sawa, hivyo wanapaswa kutiwa moyo na kupongezwa pale wanapojaribu kushiriki mijadala, shughuli za mafunzo ama kuuliza na kujibu maswali;
iv. Kutokuwa mzungumzaji mkuu na kutumia mbinu na zana zitakazowasaidia washiriki kuelewa vizuri wanachojifunza. Mbinu hizi ni pamoja na kufanya kwa vitendo zaidi, kuuliza maswali ya kupima uelewa

wa washiriki, kubadilishana uzoefu, kuhamasisha washiriki kuthamini michango ya washiriki wengine ikiwemo ubunifu na mbinu za kuamsha hamasa ili kuongeza ushiriki wa wale anao wawezesha mfano michezo na maigizo dhima;

v. Kuwa tayari kuendana na mabadiliko chanya yanayo boresha uwezeshaji ikiwemo kubadilisha eneo au mada ya mafunzo kulingana na hali halisi ya wakati huo, mfano kunapokuwa na mlipuko wa magonjwa kama vile UVIKO 19, Kipindupindu;

vi. Kutumia vichangamshi: Kichangamshi ni tendo lolote linalotolewa wakati wa mafunzo likiwa na lengo la kuamsha morali, kuelimisha, kuburudisha na kujenga mahusiano mazuri kati ya wanakikundi. Kichangamshi kinaweza kuwa ni wimbo, mchezo, kichekesho na kadhalika. Kichangamshi kitolewe wakati wowote wa mafunzo kulingana na hali ya wanakikundi (mfano kuchoka au kusinzia); na

vii. Kuzingatia muda wa kuanza na kumaliza mafunzo.

## 2.4 Utaratibu wa uwezeshaji katika Shamba Darasa la Kilimo Biashara

Utaratibu utakaotumiwa na Mwezeshaji katika kutoa mafunzo kwa wanakikundi ni:-

i. *Kufungua mafunzo:* Darasa lifunguliwe kwa utaratibu utakaokubaliwa na washiriki kwa lengo la kuamsha hamasa ya washiriki. Kwa uzoefu uliopo linaweza kufunguliwa kwa sala, wimbo, ngoma au kaulimbiu watakayojitungia kuhusu SDKB;

ii. *Mahudhurio:* Kila darasa linapoanza ni muhimu kuchukua mahudhurio ya wanakikundi wote Kila kikundi kiwe na daftari la mahudhurio ili kuhakiki ushiriki wa kila mshiriki na daftari hilo litunzwe vizuri. Mwishoni mwa msimu, mshiriki ambaye mahudhurio yake katika shughuli za SDKB yatafikia asilimia 80 na kuendelea atafuzu na kupata cheti cha ushiriki;

iii. *Mrejesho/Yatokanayo:* Kabla ya kuanza utaratibu wa siku, washiriki warejee yaliyofanyika kwenye darasa lililopita ili kama mshiriki hakuwepo au amesahau ajiweke katika hali ya kujua /kufahamu kilichotokea ikiwa ni mbinu bora ya kupata mwendelezo sahihi wa kazi/somo;

iv. *Makubaliano ya kazi ya siku husika:* Katibu aelezee kazi na taratibu za siku hiyo ili mwezeshaji waweze kujadiliana na kuelewana kabla ya kuanza utekelezaji wa kazi walizokubaliana;

v. *Kuandaa mpango kazi:* Wanakikundi wanatakiwa kukutana kulingana na mpangokazi waliouandaa katika eneo wanalofanya shughuli zao (mfano katika shamba, eneo la kuhifadhi mazao, usindikaji, shughuli za masoko na uandaaji wa lishe bora) kwa ajili ya mafunzo na kupangiana ratiba ya kukagua maendeleo ya kazi zao;

vi. *Kichangamshi:* Mwezeshaji anaweza kuhamasisha wanakikundi kutumia kichangamshi katika hatua yoyote ya mafunzo; na
vii. *Kufunga mafunzo:* Mwenyekiti atafunga mafunzo ya siku kwa kuwashukuru wajumbe na kutaja tarehe nyingine ya mafunzo.

## 2.5 Hatua za kuanzisha na kuendesha Shamba Darasa la Kilimo Biashara

Uanzishaji na uendeshaji wa SDKB utafuata hatua zifuatazo:-

### *2.5.1 Kuitisha na kufanya mkutano wa hadhara wa kuanzisha Shamba Darasa la Kilimo Biashara*

Katika maandalizi ya kuitisha na kufanya mkutano wa hadhara mwezeshaji atafanya yafuatayo:-

i. Kutoa taarifa kwa uongozi wa kijiji ili kupangiwa siku ya mkutano wa hadhara kuhusu kuanzisha SDKB. Wadau ni kama vile wauza pembejeo, wakulima, wasindikaji, wasafirishaji, wanunuzi, vikundi mbalimbali vilivyopo katika jamii, viongozi wa serikali katika jamii husika, wadau wa mandeleo, mashirika ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali na makampuni;
ii. Kuhakikisha kuwa makundi yote muhimu katika jamii (wanawake, wanaume, vijana, wenye mahitaji maalumu na wazee) yamewakilishwa katika mkutano huo kabla ya kuanza mkutano;
iii. Kufanya mkutano wa hadhara wa uhamasishaji ambapo mwezeshaji ataelezea dhana, madhumuni, manufaa, namna ya kuendesha SDKB na sifa za mtu kujiunga. Sifa hizo ni:-

- Awe mkazi wa eneo husika na anayekubalika katika jamii;
- Awe tayari kuhudhuria na kushiriki shughuli zote za SDKB kwa msimu mzima;
- Awe tayari kutoa elimu atakayoipata kwa wakulima wengine nje ya kikundi/eneo;
- Awe tayari kukubaliana na maamuzi ya wanakikundi wengi kwa mfano kuchangia michango mbalimbali ya kuendeleza shamba darasa pale inapohitajika;
- Awe mkulima mwenye uwezo wa kufanya kazi wakati wowote;
- Awe na akili timamu, nidhamu, mbunifu na kuheshimu taratibu za kikundi;
- Awe na utayari wa kutoa eneo la shamba kwa ajili ya mafunzo pale inapobidi;
- Awe tayari kutumia elimu aliyonayo na atakayoipata katika shughuli za Kilimo; na
- Awe na umri usiopungua miaka 18.

iv. Kutoa maelezo kuhusu mifumo ya ki-elektoroniki inayotumika nchini ambayo inaweza kumsaidia mkulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani kupata taarifa mbalimbali zinazohusiana na masuala ya mnyororo wa thamani katika kilimo;

v. Kutoa muda wa majadiliano, ufafanuzi, maswali na majibu ili kuwapa fursa wadau walioshiriki katika mkutano kuelewa zaidi dhana ya shamba darasa, namna ya kuanzishwa, ushiriki wao katika shamba darasa na namna ya kutumia mifumo ya ki-elektroniki iliyopo kwa ujumla.

vi. Pia ni vyema mwezeshaji ahakikishe maoni yanapatikana kutoka kwenye makundi muhimu yaliyohudhuria mkutano wa hadhara;

vii. Kuandikisha wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani waliohamasika na walio tayari kujiunga na kusaidia uanzishwaji na uendeshaji wa SDKB; na

viii. Kusimamia makubaliano ya kupanga tarehe ya kukutana na waliohamasika kwa ajili ya kuanzisha SDKB.

### *2.5.2 Kuitisha na kufanya mkutano na wadau waliohamasika kuunda kikundi cha Shamba Darasa la Kilimo Biashara*

Hatua hii itahusisha mikutano midogo midogo kadiri mwezeshaji na wanakikundi watakavyoshauriana ikiwa ni pamoja na kufanya yafuatayo:-

i. Kukutana na wakulima na wadau wengine katika mnyororo husika waliohamasika kuunda kikundi cha SDKB ;

ii. Mwezeshaji ataelezea tena kwa kina dhana, madhumuni, manufaa na namna ya kuendesha SDKB kwa wakulima na wadau wengine wa mnyororo wa thamani, kama inavyoelekezwa katika Mwongozo huu;

iii. Kuwaelekeza wadau waliohamasika wajiunge kwenye vikundi vya watu 25 hadi 30 kwa kuzingatia lengo la kikundi husika na usawa wa kijinsia; na

iv. Uchaguzi wa jina la kikundi cha shamba darasa na viongozi wake ikiwemo kamati ya maadili yenye wajumbe wapatao watano (5) kwa kuzingatia jinsia na sifa alizonazo mwanakikundi. Kiongozi atakayechaguliwa anatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

- Awe mkazi wa eneo husika;
- Awe ni mtanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18;
- Awe mwenye kujituma, busara, mwaminifu na mvumilivu;
- Awe anayekubalika na wenzake na mwadilifu;
- Awe na uwezo wa kushirikiana na wanakikundi katika kuratibu, kupanga kushawishi na kutekeleza shughuli za kikundi; na
- Awe tayari kulinda katiba ya kikundi.

### *2.5.3 Kuongoza wanakikundi kuandaa taratibu na kanuni za kuendesha kikundi.*

Mwezeshaji kuwaratibu wanakikundi kuandaa taratibu na kanuni zitakazoongoza utendaji kazi ikiwemo katiba ya kikundi.

### *2.5.4 Kuchagua zao la kujifunzia*

Mbinu ya mlinganisho kijozi itumike kuchagua zao kwa kuzingatia mchango wake katika usalama wa chakula na lishe, tija ya soko na matumizi ya bidhaa zake, kwa kufuata hatua zifuatazo:-

i. Kikundi kiorodheshe mazao muhimu yasiyozidi sita kulingana na ikolojia ya eneo na mahitaji ya soko yaliyofanyiwa utafiti na kamati ya masoko au jukwaa la kilimo;
ii. Kila mkulima achague jina la zao moja analolipendekeza kutoka kwenye orodha ya mazao waliyoyaainisha;
iii. Jedwali litengenezwe na majina ya mazao yaandikwe kwa kufuata mpangilio wa mazao unaofanana kuanzia kushoto kwenda kulia na juu kuteremka chini kama inavyoonyeshwa kwenye Jedwali Na.1.
iv. Kila wakati zishikwe kadi mbili za mazao yanayolinganishwa (moja kila mkono) na waulizwe wana kikundi lipi kati ya hayo mazao mawili ni muhimu. Zao linalotamkwa na wengi ndilo liandikwe kwenye nafasi yanapokutanika majina hayo mawili. Zoezi hilo lirudiwe mpaka mazao yote yalinganishwe ; na
v. Ihesabiwe ni mara ngapi kila zao limechaguliwa na andika alama zake. Zao litakalopata alama nyingi huwa ndilo chaguo la kikundi. Kwa mfano katika Jedwali Na. 1 zao la Alizeti ndilo chaguo namba moja la kipaumbele kwa kikundi kujifunzia katika shamba darasa.

*Jedwali Na.1 : Mfano wa Jedwali la Mlinganisho Kijozi;*

| Zao | Alizeti | Maharage | Choroko | Dengu | Mpunga | Alama | Nafasi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Alizeti | | Alizeti | Alizeti | Alizeti | Alizeti | 8 | 1 |
| Maharage | Alizeti | | Maharage | Maharage | Maharage | 6 | 2 |
| Choroko | Alizeti | Maharage | | Choroko | Choroko | 3 | 3 |
| Dengu | Alizeti | Maharage | Choroko | | Mpunga | 0 | 4 |
| Mpunga | Alizeti | Maharage | Mpunga | Mpunga | | 3 | 3 |

Ili kubaini fursa na changamoto za uzalishaji wa zao lililochaguliwa (mfano alizeti), mwezeshaji atawadodosa wanakikundi wa SDKB na kutoa ushauri juu ya mambo yafuatayo : -

i. Maandalizi ya shamba, aina ya mbegu, kiasi cha mbegu kwa ekari na upandaji;
ii. Matumizi ya mbolea, aina, kiasi kwa ekari, namna na muda wa uwekaji;
iii. Uvunaji wa mazao, muda wa kuvuna, namna ya uvunaji, kiasi cha mavuno kwa ekari ;
iv. Uelewa wa washiriki juu ya uongezaji thamani katika zao husika;
v. Upatikanaji wa masoko yenye tija, mbinu zinazotumika kutafuta masoko;
vi. Mchango wa zao husika katika usalama wa chakula na lishe bora katika Kaya;
vii. Uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika kuchagua zao; na
viii. Uelewa juu ya athari za mabadiliko ya tabianchi na matumizi ya mbinu na teknolojia himilivu kwa zao husika.

Baada ya kupata hali halisi ya mnyororo wa thamani wa zao husika, uchambuzi wa kina wa changamoto zilizopo katika zao hilo ufanyike kwa kutumia zana shirikishi ya mti wa matatizo kama ilivyoainishwa kwenye Kielelezo Na 1. Matokeo ya uchambuzi huo ndiyo yatakaotumika kwenye shamba darasa.

**Angalizo:**
Ili kuhakikisha kunakuwa na uendelevu wa SDKB ni muhimu kuhuisha na kutumia vikundi mbalimbali vilivyopo katika jamii kwa mfano vikundi vya upatu, vikundi vya kilimo na vikundi vya kuweka na kukopa (Village Saving and Loan Association - VSLA, Village Community Bank - VICOBA), Savings and Internal Lending Community – SILC).

*Kielelezo Na. 1*




Baada ya uchambuzi wa changamoto na visababishi vyake, mwezeshaji awaongoze wanakikundi kuainisha mbinu za kutatua changamoto walizozibaini kama inavyoonekana katika Kielelezo Na 2.

**Angalizo:**
Ni vizuri ikaelezwa kwamba baadhi ya vitu vina husiana kila sehemu, hivyo basi mti huu wa matatizo unapo elekezewa kwa wanakikundi inatakiwa kuuchanganua kwa undani zaidi.

*Kielelezo Na.2: Mfano wa mti wa matumaini wa uzalishaji wa zao lililochaguliwa*




**Angalizo:**
Vizuri ikaelezwa kwamba baadhi ya vitu vina husiana kila sehemu, hivyo, mti huu wamatumaini unapo elezewa kwa wanakikundi inatakiwa kuuchanganua kwa undani zaidi.

### *2.5.5 Kuongoza wanakikundi kuandaa taratibu na kanuni za kuendesha kikundi.*

Shamba Darasa la Kilimo Biashara lina sifa zifuatazo:-

i. Lisiwe na migogoro;
ii. Lenye sifa ya kujifunza teknolojia husika;
iii. Lenye ukubwa kati ya nusu ekari (0.5) hadi ekari moja(1) kwa upande wa uzalishaji mazao na kwa upande wa uongezaji thamani na masoko ukubwa wa eneo utategemea aina ya teknolojia itakayotumika.;
iv. Liwe katika ikolojia na lenye aina ya udongo unaofaa kwa zao husika; na
v. Eneo linalofikika kwa urahisi na kuonekana na wakazi wengi.

### *2.5.6 Upatikanaji na matumizi ya eneo la kujifunzia*

Taratibu za umiliki wa shamba, mapato yatokanayo na rasilimali zilizopo katika eneo husika au zilizotokana na mafunzo ziwekwe wazi kabla ya kuanza kutumia eneo husika, ikiwemo kuwa na makubaliano ya maandishi ya kutumia eneo hilo ili kuepusha migogoro kati ya mwenye eneo na wanakikundi.

### *2.5.7 Kuandaa kalenda ya msimu wa mafunzo ya SDKB*

Wanakikundi kuchambua taarifa za hali ya hewa katika eneo husika na kuandaa kalenda ya msimu na kuitekeleza. Kalenda hiyo itaainisha mtiririko wa masomo na kazi zitakazotekelezwa katika kipindi chote cha kujifunza na itakuwa ni nyenzo ya kupima mafanikio na changamoto wakati wa utekelezaji wa shamba darasa. Mwezeshaji kwa kuwezesha wanakikundi kutambua mahitaji muhimu kwa ajili ya kujifunza ikiwemo madaftari, vitini vya kanuni za kilimo bora cha zao husika, zana na pembejeo za kujifunzia. **(Rejea Kiambatisho Na.1)**

## 2.6 Uanzishaji na utunzaji wa Shamba Darasa la Kilimo Biashara

### *2.6.1. Maandalizi ya shamba*

i. Mwezeshaji kuratibu maandalizi ya shamba la kujifunzia kwa wakati kulingana na kalenda ya msimu iliyoandaliwa;
ii. Kutumia teknolojia sahihi za uandaaji wa shamba ili kuepuka athari katika udongo na wadudu rafiki; na
iii. Kugawa eneo katika sehemu kulingana na teknolojia watakazotumia kujifunza.

### *2.6.2. Maandalizi ya pembejeo za kilimo*

i. Maandalizi ya mbegu

Kuandaa mbegu/miche au vipando kwa kuzingatia ushauri wa kitaalam na ikolojia ya eneo husika ili kuleta tija. Kabla ya kupanda wanakikundi wafanye jaribio la uotaji mbegu hizo kwa kufuata hatua zifuatazo:-

- Kuchagua sehemu ya kuoteshea mbegu;
- Chagua mbegu 100 na otesha; na
- Hesabu mbegu zilizoota ili kujua asilimia ya uotaji na kufanya maamuzi ya kutumia mbegu hiyo.

ii. Matumizi ya Mbolea

Mtaalam aeleze umuhimu wa afya ya udongo na matumizi ya mbolea ili kufanya maamuzi ya aina ya mbolea na kiasi kinachohitajika. Mtaalam awaeleze makundi ya mbolea kulingana na hatua za ukuaji wa mmea. (mbolea za kupandia, kukuzia na kuzalishia)

iii. Matumizi ya viuatilifu

Mtaalam awaelekeze wakulima umuhimu wa matumizi sahihi ya viuatilifu.

### *2.6.3. Usimamizi na utunzaji wa shamba*

Wanakikundi watashiriki katika hatua zote za usimamizi na utunzaji wa shamba ikiwa ni pamoja na :-

i. Ukaguzi wa shamba;
ii. Usafi wa shamba;
iii. Uwekaji wa mbolea; na
iv. Udhibiti wa magonjwa na wadudu.

i. **Ukaguzi wa shamba**

Ili kuhakikisha washiriki wanaongeza tija katika uzalishaji wa mazao, ni muhimu mwezeshaji/mtaalam awasisitize wakulima kufuata hatua zote stahiki za ukaguzi wa shamba kwa wakati na kwa kiwango stahiki. Ukaguzi wa shamba hufanyika kwa lengo la kubaini changamoto kama vile uwepo wa wadudu waharibifu, magonjwa, magugu, upungufu wa unyevu na virutubisho ili kuchukua hatua zinazostahili kwa muda muafaka. Ukaguzi wa shamba unajumuisha vipengele vifuatavyo:

a. Uchunguzi wa mimea shambani

Uchunguzi wa mimea ufanywe na wanakikundi mara kwa mara ili kuweza kuangalia maendeleo ya mimea shambani na kubaini changamoto zinazojitokeza ambazo zinaweza kuathiri ukuaji wa mimea na hatimaye kupunguza mavuno. Uchunguzi ufanyike mapema asubuhi kabla ya jua kuwa kali kwa sababu wadudu huonekana kwa urahisi nyakati hizo. Wakati wa kufanya uchunguzi hali halisi ya shamba itatoa mwanya kwa wanakikundi kujifunza na kuamua nini cha kufanya kwa wakati muafaka.

b. Vifaa muhimu katika uchunguzi

Wakati wa uchunguzi wakulima watatakiwa kuwa na vifaa vifuatavyo: Daftari kwa ajili ya kuandikia watakayoyaona shambani, chupa kwa ajili ya kukusanyia wadudu, bango kwa ajili ya kuandikia, kalamu karatasi za manila, pini za virungu, penseli za rangi, rula, kamba, mkasi au kisu na futi kamba.

c. Uchunguzi wa Mimea

Katika shamba mimea ya kufanyia uchunguzi itachaguliwa na kuwekewa alama na namba. Mimea hiyo itafanyiwa uchunguzi mpaka mwisho wa msimu wa uzalishaji. Idadi ya mimea itakayochaguliwa kufanyiwa uchunguzi itatofautiana kutoka 10 mpaka 20 kulingana na ukubwa wa shamba na aina ya zao. Kwa mazao ya muda mfupi uchunguzi utafanyika mara moja kwa wiki na kwa mazao ya muda mrefu uchunguzi utafanyika kila baada ya wiki mbili. Rejea fomu ya uchunguzi wa mimea katika Kiambatisho Na. 3a na 3b

**Angalizo:**
Ni muhimu kufanya uchunguzi wa magonjwa, wanyama waharibifu na wadudu maadui kwa makini shambani na kuchukua tahadhari mara wanapogundulika. Wadudu na magonjwa visipodhibitiwa mapema vitaathiri mimea na kupunguza mavuno hadi kufikia asilimia 100, mfano mashambulizi ya viwavijeshi vamizi.

d. Uchambuzi wa uchunguzi wa mimea

Baada ya kumaliza kufanya uchunguzi shambani kila kikundi kikae kwenye mduara kivulini na kuchambua takwimu na taarifa walizokusanya na kutayarisha michoro. Kwenye mchoro onyesha yafuatayo: -

- Ni uchunguzi wa ngapi. Mfano wa kwanza, pili, tatu etc;
- Jina la kikundi kidogo;
- Zao husika na aina ya mbegu;
- Umri wa zao na hatua ya ukuaji;
- Hali ya hewa ya siku ya uchunguzi;
- Tarehe ya uchunguzi;
- Hali ya shamba;
- Ainisha wadudu rafiki na maadui; na
- Ainisha mimea yenye upungufu wa virutubisho.

e. Mawasilisho, Majadiliano na Maamuzi

Baada ya kumaliza uchambuzi wa takwimu na kuandaa taarifa katika vikundi vidogo Mtaalam awawongoze wanakikundi kufanya yafuatayo: -

- Kila kikundi kichague mtu wa kuwasilisha matokeo ya uchambuzi kwenye kikundi kikubwa (uchaguzi wa wawasilishaji uzingatie jinsia), na mawasilisho yafanyike kwa zamu kwa kutumia fomu ya uchunguzi Kiambatisho Na. 3a na 3b);
- Vikundi vyote vikae pamoja na kupokea mawasilisho. Wajadili mawasilisho kwa pamoja na kila mwanakikundi ashiriki kuchangia mawazo. Baadaye watafikia muafaka wa nini kifanyike, lini na nani atafanya kutokana na matokeo ya uchunguzi;
- Wakati wa majadiliano, mwezeshaji aulize maswali ya udadisi yatakayofanya wakulima wajifunze zaidi na kupata ufumbuzi wa kitaalamu;
- Kama kuna masuala yanayohitaji ufumbuzi ulio nje ya uwezo wa mwezeshaji wao, Mtaalam atoe taarifa kwa wataalam wa taasisi husika kama vile, Taasisi ya udhibiti ubora wa mbegu Tanzania

(Tanzania Official Seeds Certification Institute - TOSCI) na Mamlaka ya Udhibiti Afya ya Mimea Viuatilifu Tanzania (Tanzania Plant Health and Pestcides Authority – TPHPA) na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) kulingana na suala lililojitokeza; na

- Takwimu na taarifa za uchunguzi zitunzwe na wanapojadili taarifa za wiki walinganishe na taarifa ya wiki ya nyuma ili kupima maendeleo na mwenendo wa mazao shambani.

Mwezeshaji kutoa ufafanuzi kuhusu matokeao ya Uchunguzi uliofanyika
Baada ya mawasilisho na majadiliano mwezeshaji atoe ufafanuzi wa kitaalam kulingana na hali ya mazao. Kama shamba litakuwa na wadudu afundishe madhara ya wadudu, njia za kuwadhibiti, upatikanaji na matumizi sahihi ya viuatilifu.

**Angalizo:**
Wanakikundi wanaweza kukutana kwa dharura ili kujadili na kutatua changamoto itakayojitokeza kwenye shamba la mafunzo

f. Udhibiti wa visumbufu

Visumbufu vya mazao ni pamoja na magonjwa, wadudu, magugu na wanyama waharibifu. Kuna njia nyingi za kudhibiti visumbufu. Baadhi ya njia hizo ni; kutumia viuatilifu, viua dudu, na kufanya palizi kwa kuondoa magugu na mazingira yanayovutia uwepo wa visumbufu vya mazao na mimea.

Washiriki wanatakiwa kuwatambua na kuwahifadhi wadudu rafiki kwa kufanya yafuatayo:-

- Kutambua mahusiano ya viumbe rafiki na mazingira yake (mfano chura, buibui, nyigu n.k.) wenye uwezo wa kudhibiti wadudu waharibifu;
- Kuepuka matumizi yasiyo ya lazima ya viuatilifu katika mimea;
- Kutengeneza mazingira mazuri ya viumbe wanaoishi kwenye udongo kwa kutokuchoma moto masalia ya mazao na mimea.

Iwapo washiriki watalazimika kutumia viuatilifu katika kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao, ni vema akazingatia kanuni zote za usalama wakati wa matumizi ya viuatilifu hivyo. Mtaalam awaeleze wakulima mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kununua na kutumia viuatilifu.

g. Mwezeshaji kuahirisha mafunzo baada ya Uchunguzi

Kabla ya kuahirisha shughuli za uchunguzi katika Shamba Darasa kwanza ifanyike tathmini ya siku na kuweka mipango ya wiki inayofuata. Maoni ya wanakikundi katika mwenendo mzima wa shughuli za Shamba Darasa yatasaidia kuboresha utendaji wao katika kujifunza kwa ufanisi. Mambo muhimu ya kutathmini ni:

- Masuala yaliyofanyika kwa ubora ;
- Masuala ambayo hayakufanyika kwa ubora au yanapaswa kufanyika; na
- Jambo gani linahitaji marekebisho/maboresho.

Baada ya wanakikundi kushiriki shughuli za siku katibu atafunga kwa kutoa matangazo ya shughuli zitakazofanyika wiki/siku inayofuata ikiwemo kubaini mbinu mbalimbali za kutatua changamoto zilizoainishwa ili kutoa fursa ya kuwakaribisha wadau wengine waweze kushiriki katika utatuzi wa changamoto hizo.

Hivyo, washiriki wanapaswa kukutana kwa ajili ya palizi kulingana na maelekezo ya kitaalamu wanayopatiwa wakati wa mafunzo ya shamba darasa. Ni muhimu sana kuzingatia muda sahihi wa kufanya palizi ili kuifaya mimea iweze kukua vizuri. Pia ni vema palizi ikafanyika kabla ya kuweka mbolea ili kuepuka uhamishaji wa mbolea kutoka kwenye mche wa zao endapo palizi itafanyika baada ya kuweka mbolea.

### *2.6.4. Siku ya mkulima*

Siku ya mkulima ni siku maalum inayoandaliwa kwa ushirikiano wa wanakikundi na wataalam katika eneo husika. Siku hii inaweza kufanyika wakati wa uzalishaji, usindikaji au katika hatua nyingine yoyote kwenye mnyororo wa thamani wa zao husika. Katika siku hii wadau mbalimbali wataalikwa wakiwemo wakulima, wauza pembejeo, wasindikaji, wasafirishaji, wafanya biashara wa mazao na walaji kijijini na kutoka vijiji jirani, viongozi wa vyama mbalimbali na Serikali, wadau wa maendeleo na wataalamu mbalimbali wa maswala ya kilimo.

Lengo ni kuwawezesha washiriki wa kikundi cha SDKB kuonesha maendeleo au matokeo ya mafunzo ya shamba darasa. Pia wadau watapata fursa ya kuonesha teknolojia mbalimbali mpya zinazoweza kuwa na tija katika eneo husika. Aidha, siku hiyo inaongeza wigo kwa wakulima na wadau wengine ambao hawakushiriki katika shamba darasa kujifunza na kwenda kutekeleza katika maeneo yao.

i. Mambo ya Kuzingatia Katika Kuandaa Siku ya Mkulima

Yafuatayo ni mambo ya kuzingatia katika siku ya mkulima: -

- Matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa shughuli za shamba darasa yatajadiliwa kwa pamoja na ufumbuzi wa matatizo hayo utatolewa;
- Wakati wa kipindi cha uzalishaji siku hiyo itafanyika mara mbili, wakati mazao yakiwa katika hatua nzuri ya ukuaji (yaani wakati mazao yanaanza kukomaa) na wakati wa mavuno;
- Siku hii iwe maalumu kwa ajili ya siku ya mkulima, hivyo ni vyema isiingiliane na shughuli nyingine za kijamii katika eneo hilo mfano mnada, kliniki ya watoto na akina mama au sherehe zingine ili wanakijiji waweze kushiriki kikamilifu; na
- Pia kuwepo ngoma za asili na michezo mbalimbali zinazobeba maudhui ya siku hiyo ili kutoa burudani na hamasa kwa wale wanao tembelea maonesho hayo.
- Siku hiyo waandaliwe wakulima kueleza yaliyofanyika katika kipindi chote cha mafunzo na mafanikio yaliyo patikana.

ii. Mahitaji ya Siku ya Mkulima

Mahitaji wakati wa siku ya wakulima ni pamoja na ratiba ya matukio, mabango yanayotambulisha teknolojia zilizotumika na kuhamasisha siku ya mkulima, risala, kamera kwa ajili ya picha, burudani, chakula na vinywaji.

### *2.6.5 Uvunaji, usafirishaji, ukaushaji na uhifadhi*

i. Mahitaji ya Siku ya Mkulima

Uvunaji, ukaushaji na uhifadhi ni hatua zinazofuata mara baada mazao kukomaa shambani. Ni vizuri washiriki wakaelewa mambo wanayotakiwa kufanya wakati wa hatua hizi ili kulinda kiasi na ubora wa mazao yaliyozalishwa shambani. Mwezeshaji anatakiwa kuwasaidia wakulima kuelewa kwa kina namna sahihi ya kufanya uvunaji wa zao husika ili kulinda ubora wa zao, kuzuia upotevu wa mavuno na kufanya maandalizi sahihi kutokana na mahitaji ya soko.

ii. Ukaushaji wa mazao

Mwezeshaji awaeleze wakulima kuwa, baada ya uvunaji, ni vema mazao yakakaushwa vizuri kwa lengo la kuepusha kuvunda kwa mazao hayo endapo yatahifadhiwa yakiwa hayajakauka vizuri. Vifaa vinavyofaa kwa ajili ya kukaushia ni kama maturubai, kaushio na mikeka na ni vyema ukaushaji ukafanyika kwenye eneo salama ambapo haliwezi kuharibiwa.

iii. Uhifadhi

Uhifadhi ni hatua ya mwisho kabisa katika suala zima la uzalishaji ambapo kabla mazao hayajapelekwa sokoni ama kuongezewa thamani, washiriki wanaweza kuhifadhi mazao kwa ajili ya kuyatumia kama chakula, kusubiri bei zipande ili wauze kwa faida ama kuyahifadhi wakati wanafanya taratibu nyingine za kuyachakata ili kuyaongezea thamani kabla ya kuyapeleka sokoni.

# SURA YA TATU: KILIMO ENDELEVU

Kipengele hiki cha kilimo endelevu kinalenga kumjengea mshiriki wa SDKB maarifa kupitia mbinu shirikishi za kilimo endelevu kwa njia ya nadharia na vitendo, huku kikiangazia masuala muhimu katika mnyororo wa thamani na masuala mtambuka ambayo ni;

i. Ukaushaji wa mazao

Mwezeshaji ajadiliane na wakulima uhusiano uliopo kati ya maandalizi ya msimu na kiasi cha mavuno kwa mazao mbalimbali. Ni vema mwezeshaji akawashauri wakulima juu ya umuhimu na faida za kufanya maandalizi ya msimu mapema na kwa usahihi. Maandalizi ya msimu wa kilimo hujumuisha yafuatayo;

- Kutambua hali ya hewa ya msimu husika

Wanakikundi kwa kushirikiana na mwezeshaji wanatakiwa kuelewa tabianchi ya eneo wanaloishi ili kufanya maandalizi ya msimu mapema. Kulingana na mabadiliko ya tabianchi wanakikundi wanatakiwa kufuatilia na kupata taarifa mbalimbali za hali ya hewa zinazotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini.

**Angalizo:**
Athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi ni mtawanyiko mbaya wa mvua nyingi/ chache zitakazoathiri uzalishaji, kuharibu mimea na kuharibu miundombinu mbalimbali ya uzalishaji. Ili kukabiliana na athari hizi, wakulima wanatakiwa kupanda mbegu zinazostahimili mvua chache au mvua nyingi, kutunza na kuhifadhi mazingira na kulima kilimo himilivu kulingana na utabiri wa hali ya hewa ya msimu husika.

ii. Mbinu bora za kilimo endelevu na kuboresha afya ya udongo

Mtaalam aeleze mbinu mbalimbali za kilimo endelevu

- Matumizi ya mbolea ya mboji
- Kufanya kilimo hifadhi kwa kusumbua udongo kidogo;
- Kuacha masalia ya mazao na mimea shambani;
- Kutumia matandazo;
- Kupanda mazao yanayofunika ardhi kama vile karanga, maharage, kunde na soya;
- Kufanya kilimo mzunguko; na
- Kuchanganya mazao.

# SURA YA NNE: MASOKO

Dhana ya soko inawataka wadau katika mnyororo wa thamani wakiwemo wazalishaji, wasindikaji, wauzaji wa vyakula na wengineo kufanya shughuli zao kulingana na mahitaji ya soko. Washiriki wote wa SDKB kwa kuzingatia mahitaji ya kijinsia na makundi maalum wajengewe uwezo na uelewa wa kutosha kuhusiana na mwelekeo wa kimasoko. Hii ni pamoja na kufanya utafiti wa mahitaji ya soko ili kujua kiasi kinachohitajika, ubora unaotakiwa na wakati ambao bidhaa inahitajika kabla ya uchaguzi wa zao la uzalishaji.

## 4.1 Uundaji wa kamati ya masoko

Kamati hii itaundwa na wajumbe (3 au 5) waliochaguliwa kutoka kikundi cha shamba darasa katika eneo husika. Mjumbe atakayechaguliwa kuingia katika kamati ya masoko anapaswa kuwa na sifa zifuatazo:

i. Awe ni mkulima anayejituma;
ii. Awe ni mtu anayeweza kuwasiliana ipasavyo;
iii. Awe na uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu;
iv. Awe na uzoefu katika uongozi;
v. Awe na uwezo wa kujenga mtandao na wafanyabiashara;
vi. Awe mwaminifu;
vii. Awe na ujuzi katika biashara (awe na uwezo wa kufuatilia mwenendo wa soko).

## 4.2 Majukumu ya kamati ya masoko

Yafuatayo ni majukumu ya kamati ya masoko:-
i. Kufanya utafiti wa soko la mazao na bidhaa;
ii. Kufanya majadiliano na wanunuzi;
iii. Kutafuta fursa za masoko;
iv. Kuwasaidia washiriki wa SDKB kupanga shughuli za uzalishaji na masoko;
v. Kuwasaidia washiriki wa SDKB kukadiria gharama uzalishaji;
vi. Kutunza na kusambaza taarifa za masoko kwa washiriki wa SDKB; na
vii. Kufanya mawasiliano na wanunuzi wa mazao na bidhaa.

## 4.3 Kipindi cha kuanzisha kamati

Kamati ya masoko iundwe mara tu baada ya kikundi cha shamba darasa kuanzishwa ili kutoa muda wa kutosha kwa kamati hiyo kufanya tafiti mbalimbali za kimasoko ambazo zitasaidia katika uchaguzi wa zao la kujifunzia kwa kuzingatia fursa ya kimasoko katika zao hilo.

### *4.3.1 Namna ya kuanzisha kamati ya masoko:*

Hatua zifuatazo zinatakiwa kufuatwa katika uundaji wa kamati za masoko

i. Utangulizi: kwenye mkutano wa kikundi Mwezeshaji/afisa ugani aelezee umuhimu wa kuwa na wajumbe maalumu watakao husika na masuala ya masoko.

ii. Kuanzisha kamati ya masoko: wajumbe wawezeshwe kuamua idadi ya wajumbe na majukumu ya kamati hiyo, kulingana na ukubwa wa kikundi, wajumbe wa kamati wanaweza kuwa 3-5.

iii. Kuweka vigezo vya kuchagua wajumbe: wajumbe wanatakiwa kuweka vigezo ili kupata wajumbe wa kamati ya masoko. Vigezo hivyo ni kama kujiamini, ujuzi na uelewa wa mahesabu Pamoja na kuwa na uwezo wa kutimiza majukumu ya kamati ya masoko. Baada ya wajumbe kuchaguliwa, ni muhimu mwezeshaji afanye kikao na wajumbe wa kamati ya masoko ili kuwapa mafunzo ya namna ya kutafiti masoko na mahitaji yake.

iv. Wajumbe kujengewa uwezo wa elimu ya masoko: Wajumbe wajengewe uwezo wa utafiti wa masoko na kukokotoa gharama za uzalishaji ili waweze kupanga bei ya bidhaa zao.

## 4.4 Uchambuzi wa gharama za uzalishaji na faida

Kuwaandaa washiriki wa SDKB kufanya kilimo kibiashara, mwezeshaji anatakiwa kuwawezesha kutambua gharama za uzalishaji katika mnyororo wa thamani na mapato yanayopatikana kutokana na uzalishaji huo. Hii itasaidia kamati ya masoko kuzungumza na wafanyabiashara/walaji kuhusu bei ya soko, kutafuta fursa zilizopo na kuhakikisha wakulima wanazingatia mbinu bora za kuongeza uzalishaji. Hatua za ukadiriaji wa gharama za uzalishaji ni:-

i. Mtaalam ajadiliane na wanakikundi juu ya umuhimu wa kuchanganua gharama kuanzia uzalishaji mpaka shughuli za masoko ili kufahamu kama mazao wanayozalisha yanawaletea faida au hasara. Ni muhimu kwa wanakikundi kuelewa wapi gharama inakuwa kubwa hasa katika shughuli za uzalishaji na masoko. Hii itawasaidia kutafuta mbinu sahihi za kupunguza gharama hizo ili kupata faida zaidi;

ii. Mtaalam awawezeshe wanakikundi wa SDKB kuchagua zao moja ambalo watalitumia kuchanganua gharama za uzalishaji. Wanakikundi wanapaswa kuelewa kiasi cha uzalishaji wa zao hilo kwa msimu. Katika hatua hii, wanatakiwa kukubaliana aina ya vipimo na ukubwa wa ardhi (mfano: ekari, hekta, kilogramu au mfuko);

iii. Kwa usimamizi wa mwezeshaji, gharama zote zilizoanishwa zijumlishwe ili kupata makadirio ya gharama halisi za uzalishaji;

iv. Mwezeshaji awasaidie washiriki kukadiria kiasi cha mavuno yanayokusudiwa kuvunwa katika zao lililochaguliwa;
v. Wanakikundi watumie bei iliyopatikana kutokana na taarifa za masoko, watumie kukadiria jumla ya mapato watakayoyapata kulingana na zao hilo kukadiria jumla ya mapato; na
vi. Mwezeshaji atawasaidia wanakikundi kuweza kuchanganua jumla ya mapato yatakayopatika baada ya kutoa jumla ya gharama za uzalishaji.

*NB: Ni muhimu kuwakumbusha wanakikundi kutumia gharama halisi za uzalishaji ili kuhakikisha wanatunza kumbukumbu zitakazotumika kukokotoa gharama za uzalishaji kujua faida ya msimu husika*

Mfano wa ukokotoaji wa mapato kwa mazao (tazama Jedwali Na 2) Jedwali 2: Mfano wa Kukokotoa mapato

| Zao | Kiasi (Kilo) | Bei ya kuuzia (Tshs) | Jumla ya mapato (Tshs) |
|---|---|---|---|
| Karanga | 300 | 2,500 | 750,000 |
| Mihogo | 200 | 1,000 | 200,000 |

## 4.5 Utengenezaji wa mpango biashara kwa ajili ya masoko

Mpango biashara ni muhimu kwa kikundi kufikia malengo yake, hatua za kufuatwa katika kutayarisha mpango biashara ni pamoja na:

i. Kueleza dhana ya Mpango Biashara: Katika hatua hii mwezeshaji awawezeshe wanakikundi kuelewa yafuatayo:

- Maana ya Mapango biashara: Mwezeshaji anatakiwa kuwaeleza wanakikundi kuwa Mpango Biashara ni waraka unaaoelezea mpango wa kikundi wa namna ya kufikia malengo ya kujiendesha kibiashara. Mpango biashara, mambo yasiyotarajiwa yanayoweza kutokea kwenye biashara ya zao/ bidhaa husika na mbinu za kukabiliana nayo, hali ya kifedha ya mzalishaji na mahitaji yake ya kifedha.
- Faida za mpango biashara: ni kuwezesha uelewa na makubaliano, kuboresha taasisi na kufanya maamuzi, kuimarisha uwezo wa kifedha, kupima ufanisi, kuuza huduma/bidhaa za kikundi, kushawishi watoa fedha na wafadhili, na kurahisisha utekelezaji, ufatiliaji na tathmini ya kufikia malengo ya kikundi.

ii. Kuandaa taarifa za utafiti wa masoko: Mwezeshaji na washiriki wahakikishe kuwa taarifa zote zilizopo kwenye mpango biashara zitatokana na tafiti mbalimbali zilizofanywa na kamati za masoko.
iii. Kujaza vipengele muhimu vya Mpango Biashara: Mwezeshaji awawezeshe wanakikundi kujaza vipengele vifuatavyo vya mpango biashara: utangulizi; mpangilio wa biashara; uongezaji wa thamani; mkakati wa soko; bidhaa; vihatarishi vya soko; mpango wa kuendesha biashara; gharama za uzalishaji; vyanzo vya mapato; faida na mahitaji ya kifedha. Mwezeshaji awakumbushe wanakikundi taarifa walizonazo tayari ili ziwasaidie katika kuziweka kwenye mpango biashara ili kuwa na Mpango Biashara uliokamilika.
iv. Kuhakiki ubora wa mpango biashara: Mwezeshaji ahakikishe kila kipengele cha mpango biashara kimekalishwa ipasavyo. Mwezeshaji anatakiwa kuhakikisha kila mshiriki anaweza kutengeneza Mpango Biashara wake.

### 4.6 Kuongezea thamani bidhaa:

Uongezaji thamani wa bidhaa zinazozalishwa na wanakikundi ni wa muhimu sana ili kuifanya bidhaa kuuzika, kuhimili ushindani na kuongeza kipato kwa mkulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa zao husika. Mwezeshaji anatakiwa kuwaelekeza washirki wa SDKB kufanya yafuatayo:

i. Kupepeta na kupembua:

Baada ya kuvuna, mazao lazima yapepetwe na kupembuliwa. Lengo la kupepeta na kupembua mazao ni kuondoa wadudu, na takataka kama vile udongo, vijiti, mawe na mchanga.Upepetaji na upembuaji unatakiwa ufanyike kwa kutumia chekecheke, ungo au beseni au mashine ya kupepeta

ii. Kupanga madaraja:

Kupanga madaraja huongeza ubora na thamani ya bidhaa sokoni. Upangaji madaraja hufanyika kwa kuweka mazao na bidhaa katika madaraja mbalimbali. Madaraja yapangwe kwa kufuata ubora, ukubwa aina au rangi ya bidhaa kulingana na mahitaji ya soko.

a. Usindikaji:

Usindikaji ni namna ya kuyaongezea mazao ubora na thamani ili kuyafanya kuhimili ushindani wa soko. Usindikaji hufanyika kwa kuchakata zao ili kupata bidhaa tofauti tofauti. Usindikaji unaweza kufanyika kwa kutumia mashine ndogo au kubwa ili kupata bidhaa mahususi kama vile unga, juisi, maziwa, mafuta na nyinginezo

b. Ufungashaji na uhifadhi

Bidhaa zitokanazo na mazao zinahitajika zifungashwe kwenye vifungashio

kulingana na ujazo uliokubalika Mfano kilo 100, kilo 50, kilo 25, kilo 10, kilo 5, kilo 1, nusu kilo na robo kilo. Kabla ya kufungasha bidaha ni vema kuhakikisha vifungashio vinakuwa katika hali ya usafi na ubora unaotakiwa kwa ajili ya kulinda afya ya mlaji.

c. Kuweka chapa/lebo:

Kila bidhaa inayozalishwa na kikundi cha shamba darasa lazima ijitofautishe na bidhaa ya kikundi kingine kwa mwonekano (branding). Bidhaa inaweza kutofautishwa sokoni kwa lebo iliyotumika. Lebo juu ya kifungashio cha bidhaa lazima ionyeshe nembo ya mzalishaji na maelezo mengine ya mmiliki wa bidhaa hiyo, mfano, mahali bidhaa inapozalishwa, mawasiliano ya mzalishaji (anuani ya posta, anuani ya barua pepe na namba ya simu), jina la mmiliki au kikundi kilichozalisha bidhaa hiyo. Pia lazima lebo ionyeshe nembo ya uhalalishaji, kama "barcode" na ya ithibibati toka Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Hii inamsaidia mlaji kufuatilia ubora wa bidhaa na mahali pa kupata bidhaa hiyo.

d. Ithibati

Ithibati inatambulisha ubora wa bidhaa kulingana na viwango na kanuni zilizowekwa na taasisi ama mamlaka za kudhibiti ubora Ithibati ya mazao inatofautiana kulingalina na mahitaji ya soko, na kiwango cha ubora kinachohitajika na walaji. Mkulima anatakiwa kusajiliwa katika mfumo wa ithibati kama vile shirika linaloshughulika na mazao ya kudumu mfano chai na kahawa (RA) (Raiforest Alliance), shirika la viwango vya kimataifa (ISO) (International Standard Organisation) na shirika la biashara jumuishi (Fairtrade) na kuhakikisha anafuata taratibu zote za uzalishaji na ukaguzi zitakazoelekezwa katika taratibu za kufuata zilizowekwa na mamlaka husika kwa masoko ya ndani na nje na pia ni muhimu kufuata vigezo na taratibu vilivyowekwa na mamlaka husika ya kutoa ithibati nchini kama Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na taasisi zote zinazohusika na ukaguzi wa bidhaa na mazingira yake ya uzalishaji. Kwa mfano, ikiwa mkulima ameamua kuzalisha mazao kwa kilimo hai, anataka kupokea ithibati ya kilimo hai ambacho kinatolewa na shirika la kilimo hai Tanzania (TOAM) (Tanzania Organic Agriculture Movement). Mashirika hayo yanatoa kanuni zinazoweza kuelekeza kiwango na namna ya matumizi ya mbolea za asili, mbolea za viwandani, viuatilifu vya viwandani au asili ili kuweza kukidhi vigezo vya ukaguzi ili bidhaa ipewe ithibati.

# SURA YA TANO: LISHE BORA

Lishe bora inahusisha uwepo wa mchanganyiko wa virutibisho muhimu vinavyo hitajika kwa ajili ya kuongeza nguvu, kujenga na kulinda mwili. Ili kupata virutubisho hivyo wanakikundi wawezeshwe kuzalisha mazao katika makundi ya nafaka (wanga), Mikunde na ufugaji wa wanyama (protini), mazao ya mafuta, mbogamboga na matunda. Mchanganyiko huu utasaidia upatikanaji kwa wakati, ubora na kiasi cha viritubisho vinahitajika mwilini. Katika SDKB ni muhimu kuzingatia lishe bora ili kuimarisha afya ya jamii ili kuleta maendeleo katika jamii na nchi kwa ujumla. Hivyo lishe bora ina mahusiano ya moja kwa moja na uendelezaji wa kilimo. **(Tazama Mchoro Na. 2.)**




*Mchoro Na 2: Uhusiano kati ya lishe bora, afya na kilimo*

Katika SDKB pamoja na zao la kujifunzia wanakikunndi wahakikishe wanazalisha mazao mengine ya kuwezesha kupata virutubishi vinavyohitajika kwa ukuaji na ustawi wa jamii. Mazao hayo yazingatie upatikanaji wa makundi 5 ya vyakula yafuatayo:- vyakula vya jamii ya wanga, vyakula vya jamii ya mikunde na vyenye asili ya wanyama, vyakula jamii ya mbogamboga na matunda, vyakula vya jamii ya Mafuta, sukari na asali.

**Angalizo:**
Miongozo mbalimbali ya usalama wa chakula na Lishe inaweza kutumiwa na wawezeshaji kuongeza uelewa wa washiriki juu ya umuhimu na namna ya kuboresha lishe kupitia shamba darasa

# SURA YA SITA: MASUALA YA JINSIA

Shamba darasa linahusisha jinsi zenye umri tofauti katika kujifunza teknolojia iliyobainishwa na kundi husika. Kutokana na ukweli huo, ushirikishwaji wa jamii katika kuboresha uzalishaji, uongezaji thamani, uhakika wa soko, na usalama wa chakula na lishe ni vema makundi yote katika jamii yakashiriki kikamilifu. Makundi haya ni wanawake, wanaume na makundi maalumu, hivyo katika shughuli za SDKB washiriki wote wapewe uzito sawa katika kutoa maoni, kushiriki utekelezaji wa kazi zilizoainishwa na kunufaika na matokeo ya kazi hiyo.

Kupitia kikundi cha SDKB washiriki wanaweza kujadili kwa pamoja kuhusu masuala mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa ardhi, pembejeo, rasilimali na huduma, masuala ya lishe bora katika familia, mgawanyo wa majukumu na mapato ili kujenga uelewa na kuchukua hatua. Maelezo ya kina yameainishwa katika **Kiambatisho zana 1 -7.**

# SURA YA SABA: ZIARA YA MAFUNZO KWA WANAKIKUNDI

Wanakikundi watafanya ziara za mafunzo kwa kuwatembelea wakulima wa eneo lingine na wadau wengine katika mnyororo wa thamani kama vile wazalishaji wa mbegu, wauzaji wa zana na pembejeo, wasindikaji, wafanyabiashara na taasisi mbalimbali ili kupata taarifa na maarifa. Aidha, ziara hiyo inaweza kuwahusisha viongozi mbalimbali wanaohusika katika kuendeleza shughuli za kilimo.




Picha 1: Wanakikundi wakiwa kwenye shamba darasa

# SURA YA NANE: UFUATILIAJI NA TATHMINI WA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA

Ufuatilia na tathmini hufanyika katika kipindi chote cha uendeshaji wa SDKB kwa njia shirikishi. Tathmini hiyo inafanywa na kikundi kwa ujumla au mtu mmoja mmoja. Pia tathmini hufanyika katika maeneo ya ufanisi wa uwezeshaji, kilimo endelevu, mabadiliko ya tabianchi, uongezaji thamani, masoko, lishe, jinsia na shughuli nyingine zinazotekelezwa na kikundi husika.

Lengo la ufuatiliaji na tathmini ni kubaini ufanisi na mapungufu ya utendaji ili kufanya maboresho. Hivyo, hutoa fursa ya kuhamasisha washiriki wa SDKB na wakulima wengine kutumia njia bora za kilimo kwa msimu unaofuata. Pia huonesha maendeleo katika mchakato mzima wa mafunzo ya wakulima na makundi mengine katika mnyororo wa thamani wa zao husika. Ufuatiliaji na tathmini ushirikishe wadau wote katika mnyororo wa thamani wa zao husika wanaoshiriki kuwezesha utekelezaji wa SDKB.

## 8.1 Ufuatiliaji

Shughuli ya ufuatiliaji itafanyika kwa ushirikiano kati ya mwezeshaji na wakulima na wadau katika mnyororo wa thamani wa zao husika kwa kuangalia maendeleo ya shamba darasa. Ufuatiliaji ufanyike mara kwa mara ili kubaini mafanikio na changamoto. Wanakikundi wanatakiwa kupewa ushauri na usimamizi wa karibu zaidi ili kuwa na uelewa wa kutosha. Ushauri wa kitaalam utolewe pale unapohitajika na hii itasaidia kuimarisha vikundi ili kuvifanya viwe endelevu.

## 8.2 Tathmini

Tathmini itafanyika ili: -

i. Kupima maendeleo ya wakulima katika kutumia mbinu bora za kilimo kwa kufuata kalenda ya msimu.
ii. Kupima mabadiliko katika mavuno kutokana na kutumia mbinu bora za kilimo na matumizi ya pesa zinazopatikana ndani ya familia.
iii. Kupima matokeo ya mavuno na upatikanaji wa soko ili kujua kama kuna uwiano kati ya ubora wa mavuno na masoko.
iv. Kupima utaratibu na njia ziliotumika katika mafunzo kuona kama zimekidhi matarajio ya wakulima na wanakikundi ;
v. Kupima utendaji wa wakulima wawezeshaji waliochaguliwa kuanzisha na kuendesha mashamba darasa.
vi. Kupima matokeo na mafanikio ya matumizi ya SDKB kwa wakulima na wadau wengine katika mnyororo wa thamani wa zao ili kuongeza tija, uzalishaji, na kueneza teknolojia.
vii. Kupima maendeleo ya wanakikundi wa SDKB katika kuboresha mahusiano katika familia na kikundi, usalama wa chakula na lishe bora.

viii. Kuona kama wakulima wengine nje ya kikundi wameiga teknolojia za uzalishaji zilizotumika katika Shamba Darasa.

## 8.3 Utaratibu wa tathmini ya eneo la shamba darasa

Tathmini itafanyika kwa utaratibu ufuatao : -

i. Kupima uelewa wa wakulima katika yale waliyojifunza kupitia shamba darasa.
ii. Kupata maoni kutoka kwa wakulima walioshiriki na wakulima wengine ambao hawakushiriki katika shamba darasa;
iii. Kukagua mashamba ya wanakikundi na mashamba ya wakulima wengine waliokaribu na wanakikundi; na
iv. Kupata maoni kutoka kwa wawezeshaji wa vikundi, wataalamu na viongozi wa serikali wa eneo husika.

## 8.4 Namna ya kufanya tathmini

Ili kuleta tija katika shughuli ya tathmini zana shirikishi ya kupima utendaji (Participatory Performance Tracker -PPT) itatumika katika ngazi ya kikundi yaani SDKB na mwanakikundi binafsi katika eneo lake la uzalishaji. Tathmini inatakiwa ifanyike kabla ya kuanza shughuli za shamba darasa, kabla mazao hayajakomaa na baada ya mavuno ili kuweza kuwa na muendelezo sahihi wa upimaji wa shughuli zote za maendeleo ya wanakikundi zinazotakiwa kufanyiwa tathmini katika mnyororo wa thamani wa zao husika katika shamba darasa.

Zana hii shirikishi ya kupima matokeo inasaidia wanakikundi na afisa ugani katika:

i. Kujua hali halisi ya maendeleo ya wanakikundi katika kufuata na kutekeleza malengo waliyojipangia katika shamba darasa.
ii. Kujua mbinu waliozitumia kwa ukamilifu kati ya zile walizojifunza (adoption) na faida wanazozipata.
iii. Kupata fursa ya kujadiliana changamoto zinazowakabili katika matumizi ya mbinu (adoption) walizojifunza na kutafuta ufumbuzi ambao utawahamasisha wale ambao hawakuzitumia mbinu hizo (non adoptors) ili waweze kuzitumia msimu unaofuata.
iv. Kupanga mipango ya baadae na funzo walilolipata kutokana na tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za shamba darasa.

Zana ya ufuatiliaji na tathmini inajumuisha fomu mbili ambazo ni:

a. **Fomu ya mwanakikundi binafsi:** Fomu hii inafuatilia na kutathmini utumiaji wa mbinu mbalimbali na teknolojia katika mnyororo wa thamani wa zao husika ambalo mwanakikundi alijifunza katika SDKB. Fomu hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo zinafuatilia na kutathmini shughuli mbalimbali zilizofanyika katika msimu. Sehemu ya kwanza inatumika mwishoni mwa ukuaji wa mmea kabla ya mazao kuanza kukomaa (end of vegetative stage) na sehemu ya pili inatumika mwishoni mwa mzunguko wa zao yaani baada ya mazao kuvunwa (post harvest stage) Kiambatanisho Na 4A kinaonesha fomu inayotakiwa kutumika katika ufuatiliaji na tathmini ya mwanakikundi wa SDKB.

b. **Fomu ya kikundi:** hii inasaidia katika ufuatiliaji na tathmini ya kikundi ili kuweza kujua hali halisi ya maendeleo ya shughuli zao kulingana na malengo waliyojiwekea ambapo wataweza kuchukua hatua dhidi ya mapungufu yaliyojitokeza na kuweza kudumisha mafanikio katika kikundi. Hii ni pamoja na kufuatilia ni kwa kiasi gani wanafanya kazi kwa ushirikiano kama wanakikundi, na kupima utayari wao katika shughuli zinazofuata. Fomu hii inatumika mara mbili katika msimu mmoja wa mzunguko wa zao, ambapo kwa mara ya kwanza hutumika sambamba na fomu ya mwanakikundi binafsi mwishoni mwa msimu wa ukuaji wa mmea na mara ya pili fomu hiyo hiyo hutumika sambamba na fomu ya mwanakikundi binafsi inayotumika mwishoni mwa mzunguko wa zao baada ya mavuno.

## 8.5 Mambo ya kudodosa wakati wa kufanya tathmini

i. Ngazi ya mshiriki binafsi wa SDKB: Fomu ya ufuatiliaji na tathmini katika ngazi hii inaweza kuboreshwa kulingana na aina ya zao analozalisha mkulima. Wakati wa tathmini mwezeshaji adodose mambo yaliyoainishwa katika Kiambatisho Na: 4A

ii. Ngazi ya kikundi cha SDKB.: Wakati wa tathmini afisa ugani adodose mambo yafuatayo:

- Jina la kikundi na jumla ya idadi ya washiriki hai (wanawake wangapi na wanaume wangapi), idadi ya viongozi (wanawake wangapi na wanaume wangapi), na idadi ya washiriki wakati wa mkutano (wanawake wangapi na wanaume wangapi).
- Mafanikio ya kikundi katika masuala yafuatayo: afisa ugani anatakiwa kutengeneza swali katika ngazi ya kikundi ambalo jibu lake liwe katika madaraja yafuatayo: Mbaya Zaidi = 0 Mbaya =1,

wastani =2, nzuri = 3 na nzuri zaidi = 4. Maswali yalenge katika vipengele vifuatavyo:

i. Ujumuishaji wa kijinsia: maswali yalenge kuuliza masuala ya jinsia na usawa.
ii. Kiwango cha utekelezaji wa shughuli mbalimbali katika kikundi: maswali yalenge kuuliza yafuatayo: utekelezekaji wa kanuni na sera za kikundi ukoje? utunzaji wa kumbukumbu ukoje? mtangamano na uongozi wa kikundi ukoje?
iii. Ufanisi wa kikundi: maswali yalenge kuuliza yafuatayo: ufikiaji na upatikanaji wa pembejeo; ufikiaji na upatikanaji wa huduma za ugani; ufikiaji na utunzaji wa shamba au eneo la maonyesho; utekelezaji wa mbinu bora za kilimo katika mashamba ya washiriki wa shamba darasa, na mahusiano na vikundi vingine.
iv. Uendelevu wa shughuli: maswali yalenge kuuliza yafuatayo; mahusiano na taasisi za nje (mfano, mashirika yasiyo ya kiserikali/taasisi mbalimbali); ufikiaji na upatikanaji wa huduma za kifedha

*Kiambatisho Na. 4B kinaonesha fomu inayotakiwa kutumika katika ufuatiliaji na tathmini ya vikundi vya SDKB.*

## 8.6 Uchambuzi wa matokeo ya tathmini

Hatua zifuatazo zitatumika kuchambua matokeo ya tathmini katika ngazi ya mtu mmoja mmoja na kikundi.

i. Ngazi ya mtu mmoja mmoja
- Utangulizi na mahudhurio: afisa Ugani au mwezeshaji anatakiwa kunukuu mahudhurio ya waliopo na wasiokuwepo. Mkutano unatakiwa ufanyike katika chumba/eneo la wazi. Na mwezeshaji ahakikishe washiriki wamekaa mkao wa duara au nusu duara kuwezesha ushiriki mzuri katika uchambuzi wa tathmini.
- Kufuatilia na utekelezaji wa mbinu bora kwa mkulima mmoja mmoja: Mwezeshaji anatakiwa kuanza zoezi la tathmini kwa kuelezea madhumuni ya zoezi zima la tathmini. Hii inasaidia washiriki kupata uelewa wa zoezi linalofanyika na kukumbuka mbinu walizojifunza katika mzunguko uliopita na mafunzo waliyopata. Afisa ugani atumie lugha wanayoielewa na maneno wanayotumia katika kuuliza maswali. Pia mwezeshaji anaweza kutumia picha kuongeza uelewa na kukumbuka.

- Kuwajengea uwezo: Mwezeshaji atumie njia hii kuwajengea uwezo washiriki kwenye maeneo yaliyowapa shida katika utekelezaji wa mbinu mbalimbali. Ikitokea washiriki wachache tu ndiyo wanaotekeleza, anapaswa awaulize sababu ya kutokutekeleza na awaeleze umuhimu wa kutekeleza mbinu bora za uzalishaji.
- Kuweka madaraja: Kwa kuangalia jumla ya mbinu zilizotekelezwa na mshiriki mmoja mmoja, aweke madaraja yafuatayo ili wakulima waone wako daraja gani. Daraja A: Kama kikundi kimetekeleza mbinu bora pendekezwa kwa asilmia 76 mpaka 100; Daraja B: Kama kikundi kimetekeleza mbinu bora pendekezwa kwa asilmia 51 mpaka 75; Daraja C: Kama kikundi kimetekeleza mbinu bora pendekezwa kwa asilmia 26 mpaka 50 na Daraja D: Kama kikundi kimetekeleza mbinu bora pendekezwa kwa asilmia 0 mpaka 25. Baada ya kuona wapo daraja gani, washiriki wahamasishwe umuhimu wa kutekeleza mbinu bora za uzalishaji.

ii. Ngazi ya kikundi cha shamba darasa la kilimo biashara

- Kujichunguza: Afisa ugani anatakiwa kuwaeleza kuwa baada ya kujichunguza binafsi katika utekelezaji wa mbinu bora za kilimo sasa wajichunguze kama kikundi ni maeneo yapi wamefanikiwa katika utekelezaji. Anatakiwa kutengeneza swali katika ngazi ya kikundi ambalo jibu lake liwe katika madaraja yafuatayo: mbaya=1, wastani=2, nzuri=3 na nzuri zaidi=4. Ni muhimu swali liulizwe kwa washiriki wote na wakubaliane kwa kutoa sababu ya maamuzi ya jibu lililotolewa. Na awape nafasi kuelezea uwezo wao, udhaifu wao na mpango wao kama kikundi katika kutatua changamoto zilizojitokeza.
- Kupima ukuaji wa kikundi na tafakari: Mwezeshaji anatakiwa awape nafasi washiriki baada ya kupata matokeo ya hatua ya kwanza kujadili na kutoa sababu kwa nini maeneo fulani wana uwezo na maeneo mengine wanashindwa.
- Kutengeneza mpango kazi: Washiriki wanatakiwa kupanga namna ya kutatua na kuweka vipaumbele kwa ajili ya kuanza mzunguko mwingine wa shamba darasa. Mwezeshaji anatakiwa awapongeze wanakikundi kwa mafanikio waliyoyapata na kuwahamasisha waendelee kufanya maboresho zaidi. Mwezeshaji anapaswa kunakili maendeleo ya kipekee yaliyobainika kwa wakulima wakati wa tathmini.
- Kufunga zoezi la tathmini: Mwezeshaji anatakiwa kuwapa matokeo ya zoezi zima ili watunze kumbukumbu.
- Kushukuru: Mwisho afisa ugani anatakiwa awashukuru washiriki kwa kutenga muda wao na kushiriki kikamilifu. Baada ya hapo anatakiwa afunge zoezi la tathmini.

## 8.7 Matumizi ya uchambuzi wa matokeo ya tathmini

Uchambuzi wa matokeo ya tathmini unasaidia kupima utendaji kazi wa afisa ugani, wakulima na wadau wengine wa mnyororo wa thamani kwa ujumla. Hivyo inashauriwa kwamba pamoja na taarifa za tathmini kubakia kwa wanakikundi na afisa ugani, zitumwe katika ngazi ya juu ya afisa ugani anayesimamia shamba darasa. Hii itasaidia kujua ufanisi na mapungufu katika utendaji kazi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa kwa ajili ya maboresho.

# SURA YA TISA: KUHITIMU MAFUNZO YA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA

Mwishoni mwa msimu wa shamba darasa ikimaanisha mwisho wa hatua fulani ya mnyororo wa thamani wa zao husika wanakikundi walioshiriki katika hatua hiyo mfano uzalishaji au usindikaji watafanya mahafali ya kuhitimu mafunzo ya hatua hiyo. Wanakikundi wenye mahudhurio mazuri (kati ya asilimia 80 na100) na kuweza kutumia teknolojia walizojifunza katika maeneo wanapofanya shughuli zao mfano mashambani au eneo la usindikaji watapewa vyeti vya ushiriki. Kati ya wanakikundi watakaofuzu na kupata vyeti watachaguliwa wenye uwezo wa kuanzisha na kuendeleza Mashamba Darasa kama wakulima wawezeshaji.

Wanakikundi waliohitimu hatua ya uzalishaji ni vyema Afisa ugani akawashauri waendelee kuwafundisha wengine katika maeneo yao. Hii itasaidia kuongeza thamani ya mazao ili kuboresha upatikanaji na usalama wa chakula, soko na kuwawezesha wanakikundi kupata faida hivyo kuwawezesha kufanya kilimo endelevu na cha kibiashara.

Wakati wa kuhitimu tafrija fupi itafanyika kwa wahitimu kama motisha na kuwafanya waone fahari kwa kazi waliyoifanya kwa msimu mzima. Pia, kuwahamasisha na kuwavutia wakulima wengine kujiunga na kuanzisha vikundi vipya vya Shamba Darasa. Wakati wa mahafali wakulima washirikishwe kikamilifu katika maandalizi ili kuhakikisha mambo yote yanakwenda vizuri na kuwafanya wajue kuwa ni kazi yao.

Maandalizi ya kuhitimu Kikundi cha shamba darasa kitaunda kamati mbalimbali ili kufanikisha mambo yafuatayo ;

i. Kuanda bajeti ya tafrija fupi
ii. Kuandaa ratiba ya sherehe
iii. Kumchagua mgeni rasmi na wadau wengine wanaotakiwa kushiriki
iv. Kuandaa barua za mialiko kwa mgeni rasmi, wageni wengine, risala, mabango na machapisho mbalimbali
v. Kuandaa chakula na vinywaji
vi. Kuandaa burudani kama ngoma za asili, kwaya na muziki zenye maudhui ya siku hiyo.
vii. Kuandaa vyeti.

**Angalizo:**
Mgeni rasmi atasomewa risala na wahitimu naye atatoa nasaha zake kuhusu shamba darasa na kuwatunuku vyeti wahitimu. Mgeni rasmi anaweza kuwa Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa Diwani au mtu mwingine yeyote ambaye anaweza kuwa msaada au chachu katika kuendeleza Shamba Darasa.

# SURA YA KUMI: UENDELEVU WA MASHAMBA DARASA YA KILIMO BIASHARA

Uendelevu wa vikundi vilivyoanzishwa kupitia mashamba darasa utazingatia yafuatayo:

i. Wahitimu wahimizwe kutekeleza kwa vitendo waliojifunza kupitia SDKB;
ii. Wanakikundi waliofuzu SDKB wahamasishwe kuanzisha vikundi vingine;
iii. Wahitimu wahamasishwe kujiunga na vyama vya msingi vya ushirika kama vile AMCOS na SACCOS; na
iv. Mwezeshaji atafuatilia waliohitimu SDKB na kuona endapo wanatekeleza waliyojifunza katika mashamba yao na kuwaunganisha wakulima na watoa huduma mbalimbali. Hii itawasaidia:-
    - Kupata huduma mbalimbali kwa urahisi kama huduma za ugani;
    - Kupata zana na pembejeo bora za kilimo kwa bei nafuu; c ) Kupata soko la bidhaa wanazozalisha;
    - Kupata mitaji kwa ajili ya kuendeleza shughuli za kilimo; na
    - Kuboresha miundombinu ya mashambani kama vile barabara, mifereji ya umwagiliaji na maghala.

**Angalizo:**
Wakulima walioshiriki katika vikundi vya shamba darasa wajiunge katika vikundi vya AMCOS na SACCOS ili kuwa na nguvu ya pamoja katika kufikia soko la mazao wanayozalisha.

# VIAMBATANISHO

# KIAMBATISHO NAMBA 1: KALENDA YA MSIMU

| MUDA | UWEZESHAJI | KILIMO | MASAKO | JINSIA | LISHE | UFUATILIAJI NA TATHMINI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| KABLA YA MSIMU WA KILIMO | Kuandaa zana za kufundishia<br><br>Mwezeshaji ajielimishe juu ya sifa za mwezeshaji bora<br><br>Mwezeshaji ajielimishe mbinu za uwezeshaji watu wazima | Kutoa elimu ya kilimo bora cha mazao yaliyochaguliwa na wakulima<br><br>Uchaguzi wa shamba<br><br>Kukodi shamba<br><br>Kusafisha mashamba<br><br>Kuandaa bajeti ya kilimo ya msimu<br><br>Kutoa elimu ya utabiri wa hali ya hewa<br><br>Kutoa elimu ya KIKIMATA<br><br>Kuandaa mazingira kwa ajili ya kutoa e limu ya watu wazima<br><br>ufanya ufuatiliaji na tathmini ya mipango iliyowekwa katika shughuli za kilimo | Kubaini mahitaji ya soko<br><br>Kutafuta masoko<br><br>Kuunda kamati za masoko<br><br>Kufanya makadirio ya uzalishaji | Kutoa elimu juu ya ushiriki sawa wa wanaume na Wanawake (jinsia);<br><br>Michezo ya kugawana majukumu<br><br>Umuhimu wa wanawake kushiriki kwenye kazi za kilimo | Elimu juu ya lishe bora<br><br>Utengenezaji wa bustani za mbogamboga<br><br>Kutoa elimu ya umuhimu wa zao husika katika kuimarisha lishe | Kuandaa zana shirikishi za upimaji matokeo (PPT)<br><br>Kufanya maandalizi ya zana shirikishi ya ufuatiliaji |

| MUDA | UWEZESHAJI | KILIMO | MASAKO | JINSIA | LISHE | UFUATILIAJI NA TATHMINI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| KIPINDI CHA KUPANDA NA PALIZI YA MAZAO | Tathmini ya SDKB<br><br>Mafunzo juu ya udhibiti wa magugu<br><br>Udhibiti juimuishi wa visumbufu vya mimea Kupeana mirejesho ya zoezi la uhamasishaji | Kuweka mbolea<br><br>Kunyunyiza viuatilifu<br><br>Kutoa elimu ya upandaji kwa kuzingatia nafasi pamoja na umuhimu wa palizi<br><br>Elimu juu ya zao husika: kuandaa kalenda ya zao husika, kuchagua na kuandaa SDKB; kuandaa pembejeo (mbegu,mbolea na viuatilifu), usimamizi wa udongo na maji, tathmini ya shamba darasa | Elimu ya utafiti wa soko, kuandaa kamati ya soko; | Kufanya michezo yenye kuonesha mchango wa mwanamke nyumbani<br><br>Mifano ya michezo ni; saa ya kila siku, maelewano nyumbani na mgawanyo wa majukumu nyumbani | Kuandaa bustani za mbogamboga<br><br>Elimu ya makundi ya chakula na utapiamlo | Kuandaa zana shirikishi za upimaji matokeo |

| MUDA | UWEZESHAJI | KILIMO | MASAKO | JINSIA | LISHE | UFUATILIAJI NA TATHMINI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| KIPINDI CHA UKUAJI WA MAZAO | Kufanya maandalizi ya siku ya mkulima | Kukagua mashamba<br><br>Siku ya mkulima | Kuandaa mipango ya masoko<br><br>Kufanya utafiti wa soko<br><br>Kuchagua bidhaa na mnunuzi<br><br>Kubuni mpango wa biashara<br><br>Kufanya tathmini ya gharama za uzalishaji | Kufanya michezo yenye kuonyesha jinsi mgawanyo wa majukumu unavyo athiri utendaji wa wanaume na wanawake<br><br>Mifano ya michezo hiyo ni Pamoja na:<br><br>"Kaya kufanya maamuzi" Uchunguzi kifani:" Maamuzi ya lishe" "Kuaminiana" | Upishi wa makundi mbalimbali ya vyakula<br><br>Bustani za mbogamboga | |

| MUDA | UWEZESHAJI | KILIMO | MASAKO | JINSIA | LISHE | UFUATILIAJI NA TATHMINI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| MAVUNO YA MAZAO | Kuandaa zana za kufundishia elimu ya uvunaji<br><br>Elimu ya uvunaji kwa vitendo | Kutoa elimu ya uvunaji na uhifadhi wa mazao. | Elimu ya kuuza kwa pamoja | Kutoa elimu kuhusiana na suala la kuaminiana katika familia<br><br>Kutoa elimu kuhusiana na umuhimu wa kufanya maamuzi ya pamoja kwenye familia<br><br>Mti wa mtiririko wa fedha katika familia | Elimu ya uandaaji wa makundi ya vyakula<br><br>Kutoa elimu ya unyonyeshaji mzuri kwa watoto<br><br>Elimu ya mgawanyo wa majukumu katika familia. | Kutambua gharama za uzalishaji<br><br>Maandalizi ya PPT awamu ya pili |

| MUDA | UWEZESHAJI | KILIMO | MASAKO | JINSIA | LISHE | UFUATILIAJI NA TATHMINI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| BAADA YA MAVUNO | Kuandaa zana za kufundishia. | Kutoa elimu ya uhifadhi wa mazao.<br><br>Kutoa elimu ya udhibiti wa visumbufu vya mazao<br><br>Usimamizi wa mazao baada ya mavuno<br><br>Usimamizi wa udongo na maji shambani | Utafutaji wa masoko na u simamizi fedha<br><br>Uongezaji wa thamani katika mazao | Ushirikishwaji katika usimamizi wa mapato ngazi ya kaya<br><br>Kuwatambua wanaume wenye mtazamo chanya kwenye jamii<br><br>Kikao cha bakuli la Samaki. | Upishi wa makundi mbalimbali ya vyakula | Elimu ya namna ya kujua faida ya zao husika kwa kutukia PPT 2<br><br>Mwenendo wa kikundi (PPT 2 ) |

*NB: Ikumbukwe kuwa kalenda ya msimu itaandaliwa kulingana na ekolojia ya eneo husika.*

# KIAMBATISHO NAMBA 2: MFANO WA JEDWALI LA UKADIRIAJI WA GHARAMA ZA UZALISHAJI

| Na | Shughuli | Kipimo | Idadi | Bei | Jumla ya Gharama |
|---|---|---|---|---|---|
| | MAANDALIZI YA SHAMBA NA UPANDAJI | | | | |
| 1. | Ununuzi wa shamba | | | | |
| 2. | Kupima udongo | | | | |
| 3. | Ununuzi wa vifaa vya kilimo (majembe, panga, sururu Mambo, kamba, nk) | | | | |
| 3. | Kufyeka | | | | |
| 4. | Kung'oa visiki | | | | |
| 5. | Kuondoa miti na visiki | | | | |
| 6. | Kulima | | | | |
| 7. | Kusawazisha shamba | | | | |
| 8. | Mpangilio wa shamba | | | | |
| 9. | Uhifadhi wa udongo na maji | | | | |
| 10. | Uwekaji wa mambo (Vipimo vya shimo na mstari) | | | | |
| 11. | Kuandaa mashimo | | | | |
| 12. | Kununua na kusafirishaji wa mbegu au vipando | | | | |
| 13. | Ununuzi na usafirishaji wa mbolea | | | | |
| 15. | Kupanda | | | | |
| 16 | Unyunyiziaji wa viatilifu na uwekaji mbolea | | | | |
| | Shughuli | Kipimo | Idadi | Bei | Jumla ya Gharama |
| | UTUNZAJI WA SHAMBA | | | | |
| 17 | Kuweka matandazo | | | | |
| 18 | Kupalilia | | | | |
| 19 | Kutegemeza mmea/ Kuweka mambo | | | | |
| 20 | Kupogolea | | | | |
| 21 | Manunuzi ya pembejeo za utunzaji (Mbolea ya kukuzia , viuatilifu nk) | | | | |
| 22 | Unyunyiziaji wa viuatilifu na uwekaji mbolea ya kukuzia | | | | |
| | UVUNAJI NA USAFIRISHAJI | | | | |
| 23 | Vifaa vya Uvunaji | | | | |
| 24 | Uvunaji | | | | |
| 25 | Ukaushaji | | | | |
| | Upangaji Madaraja | | | | |
| 26 | Utunzaji | | | | |

# KIAMBATISHO NAMBA 3A: MFANO WA FOMU YA UCHUNGUZI

Jina la Kikundi : ................................................................................

Uchunguzi Na. : ................................................................................

Tarehe : ................................................................................

| **Aina ya Wadudu** | **Majina ya wadudu waliopatikana shambani** | | | | | | | | | | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | |
| Wadudu rafiki | | | | | | | | | | | |
| Wadudu waharibifu | | | | | | | | | | | |
| Maadui wa asili | | | | | | | | | | | |
| Magonjwa | | | | | | | | | | | |
| Majani ya kijani | | | | | | | | | | | |
| Majani ya njano | | | | | | | | | | | |
| Urefu wa mmea | | | | | | | | | | | |
| Matatizo mengine | | | | | | | | | | | |

Uchunguzi wa jumla : ................................................................................

Mapendekezo. : ................................................................................

# KIAMBATISHO NAMBA 3B: MFANO WA FOMU YA TAARIFA YA UCHUNGUZI

1. Zao : ............................................... Idadi ya mimea .................................
2. Aina ya mbegu : ................................................................................
3. Tarehe ya uchunguzi : ................................................................................
4. Hatua ya ukuaji : ................................................................................
5. Jina la ploti : ................................................................................
6. Jina la kikundi kidogo : ................................................................................
7. Kuchora : ................................................................................
8. Urefu wa mmea: .................................. wastani
9. Idadi ya majani: .................................. wastani
10. Idadi ya wadudu marafiki: .................................. wastani
11. Idadi ya wadudu waharibifu: ...................... wastani
12. Idadi ya majani yaliyokauka: ................ wastani
13. Idadi ya majani ya njano: ........................ wastani
14. Idadi ya majani yaliyoshambuliwa na wadudu/magonjwa: ............. Wastani
15. Idadi ya majani yaliyo na rangi zingine tofauti: ...............................wastani

# ZANA

## ZANA NA. 1: ZOEZI LA KUJADILI NA KUFANYA MAAMUZI YA MGAWANYO WAKAZI KATIKA KIKUNDI CHA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA (SDKB) NA FAMILIA

i. Wanakikundi wagawanywe katika makundi mawili ya wanaume na wanawake peke yao .
ii. Mwezeshaji awaambie washiriki kufikiria majukumu ya siku ya kawaida kwa mwanamume na mwanamke, kuanzia wanapoamka hadi wanapolala.
iii. Baada majadiliano kwenye makundi, kila kundi liwasilishe kazi yake kwa wanakikundi wote.
iv. Mlinganisho ufanyike kati ya mawasilisho ya makundi yote mawili ili kutambua kiwango cha kazi kati ya mwanamke na mwanaume. Baada ya hapo wajadiliane kuhusu hali halisi ya mgawanyo wa majukumu.
v. Baada ya majadiliano hapo juu, Mwezeshaji aendeleze majadiliano kwa kuuliza maswali yafuatayo ili kuibua masuala ya jinsia katika kushiriki shughuli za mnyororo wa thamani katika kikundi cha SDKB na familia.

- Nani anawajibika kwa kazi hiyo?
- Nani analeta mapato haya katika familia?
- Ni nani hutumia matumizi haya kwa kawaida?
- Ni nani aliye na uamuzi wa mwisho kuhusu mapato na matumizi?
- Je, mti una afya gani ?
- Ni matumizi gani ambayo ni muhimu zaidi kwa uwekezaji katika kaya na mustakabali wa familia?
- Je, matumizi yapi yana madhara au sio muhimu sana kwa afya na mustakabali wa mti?
- Ni mabadiliko gani unaweza kufanya ili kuongeza mapato (mizizi) au kupunguza baadhi ya matumizi (matawi)?

Mwezeshaji aongoze tafakari kwa wanakikundi na kuchunguza nia yao ya kutaka mabadiliko. Awaulize washiriki maswali yafuatayo:

i. Una maoni gani kuhusu muundo huu wa jumla wa majukumu kati ya mwanaume na mwanamke? Je, ungependa kubadili vipi muundo huo?

ii. Ni mabadiliko gani ungependa kuona ili kufanya hali kuwa yenye usawa zaidi?
iii. Je, kuna wanaume katika jamii hii wanaoshiriki kazi za nyumbani na wake zao? Watu wana maoni gani juu ya wanaume kama hao?
iv. Je, kuna wanawake wanaoomba kusaidiwa kazi na waume zao? Watu wanasemaje kuhusu wanawake kama hao?
v. Hatua ya kuchukua baada ya zoezi : Ni kazi gani mahususi ambayo unaweza kujaribu wiki hii nyumbani kwako ili kusaidia kusawazisha majukumu katika famílía?

Mwezeshaji ahitimishe majadiliano kwa kukazia mambo muhimu yafuatayo

i. Wanaume na wanawake wote wana uwezo wa kuwa walezi wazuri wa watoto na familia na wanaweza kuingiza mapato ya familia.
ii. Kazi ya nyumbani ni ya thamani sana na ni muhimu katika kuendeleza familia nzima.
iii. Endapo kazi za nyumbani zinagawanywa kwa usawa zaidi kati ya wanaume na wanawake, wanawake wanaweza kuwa na tija kwenye mashamba yao, kushiriki katika mikutano muhimu ya vikundi, na kuwa na afya bora.
iv. Wanaume wanaposhiriki katika kazi ya kulea, wanaweza kufurahia muda zaidi na familia, kuwa mifano mizuri kwa watoto wao, na kujisikia fahari kutunza familia ikiwemo wake zao.

## ZANA NA. 2: MBINU SHIRIKISHI YA UDHIBITI WA MAPATO NA MATUMIZI YA FAMÍLIA

Mwezeshaji awagawe wanakikundi kwenye makundi yenye mchanganyiko wa wanawake na wanaume kutegemeana na idadi ya washirki (kundi moja lisizidi watu watano)

i. Mwezeshaji aelekeze kila kundi kuoredhesha vyanzo mbalimbali vya mapato katika familia na kuruhusu kila kundi kuwasilisha vyanzo vya mapato walivyojadili mbele ya washiriki wote.
ii. Baada ya hapo mwezeshaji achuke kadi za manila mbili, kadi moja ya manila iandikwe neno " Mwanamke" na kadi ya manila ya pili iandikwe neno "Mwanaume"na kuzibadika ukutani au kuzitandaza sakafuni(chini).
iii. Mwezeshaji awaeleze wanavikundi waweke vyanzo vya mapato vinavyo milikiwa na mwanamke kwenye kadi ya manila ya mwanamke na vyanzo vya mapato vinavyodhibitiwa na mwanaume kwenye kadi ya manila ya Mwanaume
iv. Mwezeshaji awaulize washiriki kuangalia hali utofauti wa udhibiti wa mapato katika familia, je wameona nini?, Kwanini hali iko hivyo? Je, nani anayefanya udhibiti wa mapato kwa kiasi kikubwa katika familia kati ya mwanamme na mwanamke, Je, kuna fursa ya majadiliano ya namna ya kuweka usawa katika udhibiti wa mapato ya família?

Mwezeshaji ahitimishe majadiliano kwa kukazia mambo muhimu yafuatayo

i. Nani anahusika katika kupata na kupanga mapato katika kaya? Je, kazi ya kulipwa inathaminiwaje ?
ii. Nani anahusika katika kulima mazao ya chakula ? Je, shughuli hizi zinathaminiwa vipi ?
iii. Ni nani anayehusika katika utunzaji wa familia na shughuli za nyumbani ? Je, shughuli hizi zinathaminiwa vipi ?
iv. Je, nini kingetokea ikiwa shughuli hizi za kutoa matunzo nyumbani zitasimama kwa siku moja au siku kadhaa ?
v. Je, ulezi wa watoto na familia kwa ujumla ni "Kazi"? Je, ni rahisi?
vi. Ni nani anapata muda mwingi wa kulala, kupumzika na burudani? Kwa nini?

## ZANA NA. 3: MBINU SHIRIKISHI YA UDHIBITI WA MAPATO NA MATUMIZI YA FAMÍLIA

Mwezeshaji awasomee hadithi hii kwa sauti au amwelekeze mshiriki wa SDKB kusoma hadithi mbele ya washiriki wote. Msomaji wa hadithi arudie mara 2-3 ili kusaidia washiriki kuelewa vizuri.

**Hadithi ya Kaya ya Zuhura na Mume wake**

*Zuhura alikuwa na shauku ya kujiunga na kikundi cha mkopo, kwa sababu alitaka kuwekeza katika baadhi ya zana ili kurahisisha uzalishaji wake, na alitaka kupanua uzalishaji wa aina mbalimbali za karanga ambazo zilihitajika sokoni. Mume wa Zuhura alimpa kianzio cha mtaji, lakini ilipofika zamu yake kuchukua mkopo wa kikundi, mme wake alichukua mkopo huo na kuuwekeza katika uzalishaji wake wa mifugo. Zuhura kila alipojaribu kumwomba mumewe arudishe, mumewe alimkemea na kusema ni pesa zake maana alimpa kianzio. Pia alisema shughuli zake ni muhimu zaidi kwa sababu yeye ndiye mkuu wa kaya. Zuhura tayari amekosa marejesho mara tatu kwenye kikundi na ameanza kuona aibu.*

*Zuhura alifanya kazi kwa bidii kwenye mazao yake na akapata mavuno mengi. Walakini, mwisho wa msimu, ni mume wake ambaye alipeleka sokoni. Baada ya kupata pesa, alizigawa kadiri alivyoona ni vema. Alitumia nyingine kulipa mikopo yake mwenyewe, nyiingine kununua malisho ya mifugo, na nyiingine kwa burudani. Zilizobaki alimpa Zuhura kwa ajili ya ada ya shule ya watoto. Ilipofika wakati wa msimu wa kilimo, Zuhura hakuweza kupata mtaji wa kuwekeza katika malengo yake ya kununua zana za kilimo na kuongeza uzalishaji kama aliyokuwa amejiwekea.*

Baada ya kusoma hadithi mwezeshaji aongoze majadailino kwa kufuata maswali yafuatayo:

1. Tatizo ni nini katika hadithi?
2. Mhusika alitarajia kupata nini?
3. Mhusika alijaribuje kutumia maarifa mapya katika kuongeza uzalishaji wa shughuli yake?
4. Ni nini kilimzuia kufaulu?
5. Je, aina hii ya matukio pia hutokea katika jamii yetu? Kwa nini?
6. Je, kuna yeyote ndani ya kikundi chetu ambaye anakumbana na matatizo haya? Mwezeshaji asilazimishe kama washiriki wanaona hofu kutoa uzoefu wao, suala hili limejikita katika mizizi ya mila na desturi hivyo washiriki wanaweza kuona shida kutoa uzoefu.

7. Je, wanakabiliana vipi na masuala haya?
8. Tunaweza kufanya nini ili kubadili hali hiyo?

Mwezeshaji anaweza kuhitimisha kwa kusisitiza kuwa, udhibiti wa mapato ya familia ni vema ukawa shirikishi ili kuondoa migogoro katika familia.

## ZANA NA. 4: PICHA YA MTI INAYOONYESHA AFYA YA BAJETI YA FAMILIA

Mwezeshaji awaeleze wanakikundi kwamba ataonyesha picha ya mti unaoonyesha afya ya bajeti ya familia, na jinsi família inavyoisimamia (mwezeshaji awaonyeshe mti kama unavyooneka katika picha hapo chini) kisha aweleze wanakikundi kuwa;

Mti unawakilisha hali ya kifedha ya kaya/familia. Mizizi inawakilisha shughuli zote zinazoleta chakula na mapato katika kaya. Mizizi mirefu na minene inawakilisha vyanzo muhimu vya mapato.

Juu ya mti (matawi marefu na mafupi) yanawakilisha matumizi tofauti tofauti katika familia. Matawi ya juu zaidi/ marefu zaidi yanawakilisha matumizi muhimu au (ya lazima) sana na matawi mafupi/ya chini yanawakilisha matumizi yasiyo ya lazima. Baada ya hapo:



i. Mwezeshaji awagawe washiriki katika vikundi tofauti (wanaume na wanawake), na awaambie wachore mti wao wenyewe, wakiweka alama kwenye mizizi yenye vyanzo mbalimbali vya mapato na matawi pamoja na matumizi yote yanayofanywa katika kaya.
ii. Mwezeshaji awaulize washiriki maswali haya yanayohusu mizizi na matawi ya mti ( vyanzo vya mapato na matumizi)
iii. Mwezeshaji awezeshe makundi kujadili mahitaji ya pesa shindani na jinsi familia hufanya maamuzi kuhusu nini cha kutumia, awaulize maswali haya ;

- Nani anaonekana kuchangia mapato (mizizi)? Nani anaonekana kudhibiti matumizi (matawi)? Kwanini inakuwa hivyo?
- Je, ni matumizi gani ambayo wanawake wanaweza kufanya peke yao? Kwa nini?
- Ni matumizi gani ambayo wanawake kwa ujumla hawana ushawishi mkubwa juu yake? Kwanini hivyo?
- Ni maeneo gani ya kutoelewana kuhusu fedha? Je, mijadala hii hutatuliwa vipi?
- Kwa kutazama picha hii, ni mabadiliko gani kama yapo ungependa kuona jinsi maamuzi yanavyofanywa?

iv. Baada ya majadiliano kwenye vikundi, mwezeshaji avilete vikundi pamoja na kila kikundi kiwasilishe michoro yake na mijadala yake. Mwezeshaji awaulize washiriki maswali yafuatayo :
- Je, miti inafananaje?
- Wanaume na wanawake wanakubaliana wapi? Vipaumbele vyao ni tofauti wapi?
- Je, unaona nini kuhusu michango ya wanaume na wanawake kwa mapato ya fedha taslimu? Nini kingetokea kwa afya ya mti ikiwa wanawake hawakuwepo ?
- Unaona nini kuhusu uwepo wa wanawake katika kiwango cha matumizi? Je, afya ya mti ingeboreshwa vipi ikiwa wanawake wangewakilishwa sawa katika kilele cha mti?

Mwezeshaji ahitimishe mjadala kwa kusisitiza umuhimu wa michango ya wanawake kwa ustawi wa kifedha wa kaya na umuhimu wa kutathmini kwa pamoja vipaumbele vya familia.Wanawake na wanaume ni muhimu kukubaliana juu ya vipaumbele sawa, mfano ni matumizi gani ya lazima na yasiyo ya lazima na kufanya maamuzi ya pamoja.

Mwezeshaji asisitize kuwa Wanawake wana taarifa nyingi kuhusu kile kinachotokea ndani ya kaya / familia kuhusu watoto, matumizi na mahitaji; tunaposikiliza mitazamo na mahitaji ya kila mmoja wetu, tunaweza kufanya maamuzi bora. Vyanzo vingi vya mapato (chini ya mti) vinasimamiwa na wanawake; uwekezaji katika njia hizi unaweza kuboresha afya ya mti (familia/kaya) na kuondoa migogoro ya familia.

## ZANA NA. 5: ZOEZI LA NAMNA SHIRIKISHI YA KUFANYA MAAMUZI KATIKA FAMÍLIA NA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA (SDKB)

i. Mwezeshaji aanze kwa kuwaeleza wanakikundi kuwa katika mjadala huu maamuzi yanayofanywa kwenye famÍlia yatachunguzwa ili kujua maamuzi hayo ni yapi, nani anayafanya, na yanafanywaje.

ii. Katika vikundi vyenye mchanganyiko wa wanaume na wanawake, mwezeshaji awaambie washiriki kutafakari orodha ya maamuzi(12-15) muhimu ambayo yanahitajika kufanywa na wanakaya. Waandike uamuzi mmoja kwa kila kadi ya manila. Mwezeshaji anaweza kutaja mifano ya uamuzi( kununua shamba, kuoa, kununua usafiri) ili kusadia zoezi kuwa rahisi.

iii. Mwezeshaji aandike Kwenye kadi tatu tofauti maneno yafuatayo:

- Mwanamke peke yake
- Mwanaume peke yake
- Mwanamke na mwanaume pamoja

iv. Mwezeshaji awaambie washiriki wajadili kila kadi (kutoka kadi 12-15 tofauti za maamuzi) na kuiweka chini ya mojawapo ya lebo tatu (mwanamke peke yake, mwanaume peke yake au mwanamke na mwanaume pamoja) kulingana na nani anafanya uamuzi huo katika kaya.

v. Kwa kutumia maswali yafuatayo hapo chini, Mwezeshaji awezeshe mjadala. Kwa kuangalia idadi ya kadi kwa kila lebo, nani anafanya maamuzi zaidi? (Hesabu maamuzi katika kila lebo). Pia Mwezeshaji adodose kwa kina kuhusiana na maamuzi kwa kila lebo kwa kuuliza maswali yafuatayo:

- **Lebo ya “mwanaume pekee”:**
    a. Haya ni maamuzi ya aina gani?
    b. Kwa nini maamuzi haya kwa kawaida hufanywa na mwanaume pekee?
    c. Nini kinatokea ikiwa mwenzi wa ndoa hakubaliani na uamuzi huu?

- **Lebo ya "mwanamke pekee":**
  a. Haya ni maamuzi ya aina gani?
  b. Kwa nini maamuzi haya hufanywa na mwanamke pekee?
  c. Je, nini kitatokea ikiwa mwenzi hakubaliani na uamuzi huu?
- **Lebo ya mwamke na mwanamume pamoja":**
  a. Haya ni maamuzi ya aina gani?
  b. Kwa nini maamuzi haya kwa kawaida lazima yafanywe pamoja?
  c. Je, nini hutokea wapenzi wanapotofautiana

vi. Mwezeshaji aulize mfano wa mojawapo ya maamuzi ya "wanawake na wanaume pamoja" ambapo washiriki walitofautiana au walikuwa na ugumu wa kufikia makubaliano:

- Aina gani ya uamuzi
- Nani alihusika katika kutoa uamuzi ?
- Je, hatimaye makubaliano gani mlifikia?
- Je, unahisi ulikuwa na sauti sawa katika uamuzi ? Kama ndio au siyo, ni kwa nini ?
- Je, kila mtu alifurahishwa na matokeo ya uamuzi huo?

vii. Mwezeshaji awaulize washiriki mfano mmojawapo wa "maamuzi ya pamoja" muhimu ambapo washirika wote walikuwa na sauti sawa katika mchakato - na kufikia makubaliano.

viii. Mwezeshaji awaulize wanakikundi wana maoni gani kuhusu mtindo wa kufanya maamuzi ambao umeelezewa hapo juu? Ni kadi gani wangependa kuhama kutoka lebo moja hadi nyingine? (Ruhusu washiriki kuhamisha kadi kwenye lebo tofauti tofauti.

ix. Mwezeshaji alete vikundi vyote pamoja na kisha aruhusu kila kikundi kwa dakika 5-10 kushiriki mjadala wao huku kundi jingine likisikiliza. Maswali yafuatayo yatasaidia katika kuongoza mjadala.

- Ni nini kilikushangaza kuhusu wasilisho la kikundi kingine?
- Je, kuna ufanano gani kati ya majadiliano toka kikundi kimoja hadi kingine?
- Je, kuna hatari au madhara gani katika familia endapo mtu mmoja atafanya maamuzi bila kuheshimu maoni ya wengine?
- Je, kuna faida gani katika familia ambayo wenzi wote wawili wana sauti sawa katika uamuzi?

x. Ili Kuiweka katika vitendo: Mwezeshaji awaambie washiriki wageukiane na kujadili angalau badiliko moja ambalo wanawake na wanaume wangependa kuona katika suala la kufanya maamuzi. Maswali yafuatayo yatasaidia katika kuongoza mjadala.

- Je, mchakato wa kufanya maamuzi ya kuridhisha mwanamke na mwanaume unatakiwa uweje?
- Unawezaje kuanza kufanya mabadiliko haya?
- Ni hatua gani ndogo utachukua wiki hii kufanya mazoezi haya?

Mwezeshaji ahitimishe mjadala kwa kueleza kuwa, ndani ya kaya moja, wanawake wakati mwingine wana mitazamo tofauti, mahitaji tofauti, na taarifa tofauti kuliko wanaume. Habari hii ni muhimu kwa kufanya maamuzi yenye manufaa kwa kila mtu katika familia. Wanawake pia hutoa mchango mkubwa katika mapato na matunzo ya familia; hivyo wana haki ya kushiriki katika maamuzi muhimu. Ni vema kufanya maamuzi shirikishi katika familia.

# ZANA NA. 6: FOMU YA UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MWANAKIKUNDI WA SHAMBA DARASA LA KILIMO BIASHARA

| | **Aina ya technolojia au mbinu bora walio tumia** | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Na** | **Jina la Mkulima** | **Kupanda kwa mistari** | **Kupanda kwa wakati** | **Mboji** | **Mbegu bora** | **Kilimo Hifadhi** | **Palizi kwa wakati** | **udhibit wa visumbufu** | **kuvuna kwa wakati** | **Jumla ya alama** | **Maoni** |
| 1 | Alfei Maseke | x | x | x | | | | x | x | 3 | |
| 2 | Alexander Chongoma | | | | x | x | x | | | 5 | |
| 3 | Masanja Habib | | | | | | | | | 8 | |
| 4 | Christina John | | | | | | | | | 8 | |
| 5 | Ramadhani Lissu | | | | | | x | x | x | 5 | |
| 6 | Daniel Luther | x | x | x | x | x | x | x | | 1 | |
| 7 | Avitha Byampanju | x | x | x | | x | x | x | | 1 | |
| 8 | Matungwa Bagwerwa | x | x | x | x | x | x | x | | 1 | |
| 9 | Edward Charles | | | | x | x | | | | 5 | |




Wizara ya Kilimo

Mji wa Serikali, Mtumba

S.L.P 2182, Dodoma, Tanzania

Simu: +255 733 800 200

Nukushi: +255 (026) 2320037

Barua pepe: ps@kilimo.go.tz